# PESA ZIKO WAPI?

Utozaji Kodi na Hali ya Utekelezaji wa Dira ya Madini ya Afrika Nchini Tanzania

Tax Justice Network – Africa

Julai 2016

# SHUKURANI


## Pesa Ziko Wapi?

Utozaji kodi na hali ya utekelezaji wa Dira ya Madini ya Afrika: Utafiti mahsusi nchini Tanzania na Afrika Mashariki
Mwandishi: Alhassan Atta-Quayson.

Chapisho hili limekamilishwa chini ya usimamizi wa Cephas Makunike. Pia limenufaika kutokana na maoni ya Alvin Mosioma na Kwesi W. Obeng. Ripoti hii imefanyiwa mapitio na Dr. Abdulai Darimani na Sylvester Bagooro. Dr. Tom Odhiambo alihariri taarifa za ripoti hii.

Chapisho hili limewezeshwa na msaada wa fedha toka Oxfam IBIS. Hata hivyo, maoni yaliyotolewa hapa siyo lazima yaakisi msimamo wao rasmi kisera.

Yaliyomo katika chapisho hili ni wajibu pekee wa Tax Justice Network-Africa


## Kuhusu Sisi

Tax Justice Network-Africa (TJN-A) (Mtandao wa Haki Kodi –Afrika) ni Asasi ya Afrika na ni mwanachama wa Muungano wa Kiulimwengu wa Kodi ya Haki (Global Alliance for Tax Justice (GATJ).

Dira yetu ni "Afrika mpya ambapo haki ya kodi inashamiri na kuchangia katika maendeleo ya haki sawa, shirikishi na endelevu."

Sambamba na mamlaka tuliyodhaminiwa, dhima ya TJN-A ni "Kuongoza katika mapambano ya kupatikana haki katika kodi kwa ajili ya maendeleo ya Afrika ili kuwezesha wananchi na taasisi kukuza mifumo ya kodi inayozingatia haki sawa kwa njia za utafiti, kukuza uwezo na ushawishi wa sera."

TJN-A kwa sasa ina wanachama 29 katika nchi Afrika. Wanachama wanakuwa kama kitovu cha kutekeleza kazi za haki kodi katika nchi zao na mara nyingi wanaongoza majukwaa yanayoshirikisha asasi nyingi zenye ari ya kushiriki au ambazo ni wadau katika kampeni ya haki kodi.


Imetafsiriwa na kuchapishwa na Policy Forum.

# YALIYOMO

Shukurani ..... ii

Orodha ya Jedwali ..... iii

Orodha ya Chati ..... iii

Orodha ya Vifupisho ..... iv

Muhtasari ..... v

**1. UTANGULIZI** ..... 1
1.1 Usuli ..... 1
1.2 Malengo ya Utafiti ..... 1
1.3 Mbinu za Utafiti ..... 1

**2. DIRA YA MADINI YA AFRIKA (AMV) – MASHARTI YA MSINGI KATIKA UTAWALA WA FEDHA NA MAPATO KATIKA SEKTA YA MADINI TANZANIA** ..... 3

**3. MAELEZO MAFUPI YA SEKTA YA MADINI TANZANIA** ..... 7

**4. MAELEZO MAFUPI YA UTAWALA WA FEDHA KATIKA SEKTA YA MADINI TANZANIA** ..... 11

**5. USIMAMIZI WA MATUMIZI YA MAPATO KATIKA SEKTA YA MADINI TANZANIA** ..... 13
5.1 Taasisi Muhimu zenye Wajibu katika Usimamizi wa Matumizi ya Sekta ya Mapato ..... 13
5.1.1 Wizara ya Nishati na Madini ..... 13
5.1.2 Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania ( (TMAA) ..... 13
5.1.3 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ..... 13
5.2 Mipango Mingine ya Usimamizi wa Mapato ..... 13
5.2.1 Mikataba ya Maendeleo ya Madini (MDAs) ..... 13
5.2.2 Uwazi katika Matumizi ya Mapato ya Sekta ya Madini ..... 14
5.2.3 Mikataba ya Uwekezaji wa Nchi Mbili (BITs) na Mikataba ya Tozo la kodi maradufu (DTTs) ..... 14
5.2.4 Manufaa ya Jamii Kutokana na Madini ..... 14
5.2.5 Mfuko maalumu wa matumizi ya mapato ..... 15

**6. MWONGOZO WA JUMUIYA YA AFRIKA YA MASHARIKI KWA SEKTA YA MADINI** ..... 16

**7. TATHMINI: KUOANISHA NA KUPANGA KWA KINA AMV KATIKA NGAZI YA TAIFA** ..... 17
7.1 Kuoanisha na Kupanga kwa Kina Utawala wa Fedha za Madini Tanzania ..... 17
7.2 Kuoanisha na Kupanga kwa Kina Usimamizi wa Matumizi ya Mapato Tanzania ..... 20

**8. TATHMINI: KUOANISHA NA KUPANGA KWA KINA AMV KATIKA NGAZI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI** ..... 22

**9. HITIMISHO** ..... 23

**10. MAPENDEKEZO** ..... 24

**MAREJEO** ..... 25

**VIAMBATANISHO** ..... 26
Kiambatanisho 1: Maelezo ya Jinsi Uchunguzi wa AMV Ulivyofanyika Tanzania ..... 26
Kiambatanisho 2: Kadi ya Alama Kuhusu Kiwango cha Utekelezaji wa AMV Tanzania ..... 27

**Orodha ya Jedwali**

Jendwali 1: Mikakati ya Utawala wa Fedha na Usimamizi wa Mapato kwa Sekta ya Madini chini ya AMV kwa Ngazi ya Taifa ..... 5
Jedwali 2: Mikakati ya Utawala wa Fedha na Usimamizi wa Mapato kwa Sekta ya Madini chini ya AMV kwa Ngazi ya Kanda ..... 6
Jedwali 3: Mchango wa Migodi tisa ya Madini katika Jumla ya mapato ya Kodi Tanzania Bara ..... 8

**Orodha ya Chati**

Chati1: Historia ya Mauzo ya Madini Kutoka Migodi Mikubwa (1999 - 2014) ..... 8

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AMDC | Kituo cha Maendeleo ya Madini Africa (African Minerals Development Centre) |
| AMV | Dira ya Madini ya Afrika (Africa Mining Vision) |
| AU | Umoja wa Afrika (African Union) |
| BITs | Mikataba ya Uwekezaji wa Nchi Mbili (Bilateral Investment Treaties |
| CSR | Jukumu la Ushirika wa Kijamii (Corporate Social Responsibility) |
| DTTs | Mikataba ya Tozo ya Kodi Maradufu(Double Taxation Treaties) |
| EAC | Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (East African Community) |
| EITI | Mpango wa Uwazi wa Tasnia vya Uziduaji (Extractive Industries Transparency Initiative) |
| GDP | Zao Ghafi la Ndani (Pato la Taifa) (Gross Domestic Product) |
| MDAs | Mikataba ya Uchimbaji wa Madini (Mining Development Agreements) |
| MoEM | Wizara ya Nishati na Madini (Ministry of Energy and Minerals) |
| RECs | Jamii za Uchumi za Kikanda (Regional Economic Communities) |
| TEITI | Mpango wa Uwazi wa Viwanda / Tasnia vya Uziduaji Tanzania (Tanzania Extractive Industries Initiative) |
| TMAA | Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania (Tanzania Minerals Audit Agency) |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority) |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani (Value Added Tax) |
| NEPAD | Ushirikiano Mpya kwa Maendeleo ya Afrika (New Partnership for Africa's Development) |

# MUHTASARI

Utafiti huu unatathmini usimamizi wa sasa wa sekta ya madini nchini Tanzania, pamoja na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (Jumuiya ya Afrika MasharikiEAC) kwa kuzingatia hasa utawala wa fedha pamoja na usimamizi wa matumizi ya mapato. Tathmini imefanyika ili kuonyesha mapungufu kati ya malengo ya Dira ya Madini ya Afrika (AMV) na kinachotokea hivi sasa Tanzania (na Jumuiya ya Afrika Mashariki). Malengo ya utafiti ni kutathmini upungufu kati ya hali ilivyo katika ngazi ya kitaifa na ya kikanda kwa kulinganisha na kile AMV inachokusudia, ili kutoa mapendekezo ya maeneo yanayohitaji kushughulikiwa. Utafiti unatumia viashiria vya utafiti, kama vilivyoainishwa katika 'Mpango wa Utekelezaji wa AMV' wa Desemba 2011, kama kigezo au alama teule (benchmark).

Utafiti unaonyesha kuwa kadiri miaka inavyopita, Tanzania imeboresha uwezo wake kitaifa wa kukagua uzalishaji wa madini na uuzaji nje ya nchi kwa kuanzisha shirika pekee lililopewa wadhifa wa ukaguzi wa madini, Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA). Matokeo yake ni kwamba, madeni ya kodi ambazo hazijalipwa yaliainishwa, wakati pia ikisaidia kujenga uwezo wa makampuni ya madini kukokotoa mapato ya kodi yanayotakiwa kulipwa. Kufuatia kuanzishwa kwa Sera ya Madini ya mwaka 2009, Tanzania pia imefanya mabadiliko katika mfumo wa kodi ili kuongeza mapato yanayotokana na sekta ya madini, ambayo imeshuhudia mchango wa mapato yanayotokana na kodi ya madini kwa kulinganisha na jumla ya mapato ya kodi zote ikiongezeka toka asilimia 2.41 mwaka 2001 hadi asilimia 4.41 mwaka 2014.

Pia kumekuwa na shughuli za kuwajengea uwezo watumishi wa Serikali kujadili mikataba ya madini na kufuatilia udhibiti ili kuhakikisha kuwa kanuni/sheria zilizowekwa zinafuatwa, Kituo cha Maendeleo ya Madini Afrika (AMDC), taasisi iliyoanzishwa ili kuhakiki utekelezaji wa yaliyoainishwa katika AMV pia kikishiriki kikamilifu. Miongozo ya uhawilishaji bei iliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na mipango mbalimbali ya TMAA pia imesaidia kupunguza upotevu unaotokana na uvujaji haramu wa fedha kutoka sekta ya madini.

Tanzania bado inahitaji kuchukua hatua zaidi kuhusu kufanya mapitio ya mikataba ya tozo la kodi maradufu na Mikataba ya Uwekezaji wa Nchi Mbili (BITs) ambazo Tanzania imekubaliana na kutiliana sahihi na nchi wenyeji wa makampuni ya madini. Kuna uwezekano kwamba nchi ilipoteza haki ya kutoza kodi kwa wawekezaji kwani utawala umekuwa ukiwalinda sana wawekezaji. Kwa nyongeza, mtindo unaotumika katika kujadili mikataba ya uchimbaji madini (MDA) nao unaonekana kuwa na matokeo yanayompendelea mwekezaji zaidi kuliko Serikali, hivyo kupunguza mapato.

Kuhusu usimamizi wa matumizi ya sekta ya madini, Tanzania, sasa iko katika hatua za kukamilisha uanzishaji wa mfuko maalumu wa matumizi ya mapato yatokanayo na sekta ya gesi. Hata hivyo kuna haja pia ya kuanzisha mifuko huru ya kiuchumi kwa ajili ya madini mengine kwa kuwa hizi ni rasilimali zinazoisha, kwa hiyo inapasa pia kuzingatia mahitaji ya vizazi vijavyo. Licha ya hayo, Tanzania haina mkakati wa kisera wa kuhimiza makampuni ya uchimbaji madini kutoa kipaumbele kwa jamii ya Kitanzania katika uamuzi wowote unaohusu ajira na hakuna utaratibu wowote unaozitaka kampuni hizi kutumia sehemu ya pato lao katika kuwekeza kwenye jamii ili kuimarisha afya, elimu na miundo mbinu kwa ujumla.

Katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, mikakati katika ngazi ya kanda imezuiwa na kutokuwa na mwafaka miongoni mwa nchi washirika kuhusu mkakati wa sekta ya madini. Matokeo yake, juhudi za sasa katika ngazi ya kanda haziendi sambamba na matarajio ya AMV kuhusu usimamizi wa fedha kwa ujumla na matumizi ya mapato ya sekta ya madini, ingawaje kuna juhudi zinazofanyika katika ngazi ya sekretarieti ambazo zinafaa kupongezwa.

Kutokana na matokeo ya utafiti, mapendekezo yafuatayo yanatolewa kwa ngazi ya taifa, asasi za kiraia kama vile Mtandao wa Haki Kodi-Afrika (Tax Justice Network-Africa) zinaweza kutumia mapendekezo haya pia katika mipango yao ya utetezi miongoni mwa wadau wasiohusika na sekta ya madini.

i. Tanzania inahitaji kuendeleza juhudi za sasa za kuandaa dira ya taifa ya uchimbaji madini inayofungamana na Dira ya Uchimbaji Madini ya Afrika (AMV). Kasi inayotokana na juhudi zinazofanyika katika ngazi ya Serikali kwa kushirikiana na AMDC zisipotee. Asasi za kiraia zinaweza pia kuunda mipango yao kuendana na AMV ili kuendeleza juhudi zilizokwisha anza;

ii. Tanzania inahitaji kuendelea kuhakikisha kuwa uwezo wa ukaguzi wa madini ambao TMAA inayo tayari unakuzwa kila wakati ili uwezo wa ukaguzi uendane na mikakati inayoendelea kujitokeza kuhusu uvujaji haramu ya fedha katika sekta ya madini. Kuna haja ya kuhamasisha wadau wote kuhusu uimarishaji huu:

iii.

iv. Tanzania sharti iendelee kutumia AMDC katika maeneo mengine kuhusu mapato ya sekta ya madini, ikijumuisha uwezo wa kujadili makubaliano yanayohusu madini pamoja na mfumo wa utawala ulio bora kuhusu BITs na mikataba ya tozo la kodi maradufu (DTTs) kuhakikisha kwamba nchi inapata mfumo wa uchimbaji madini ulio bora zaidi kama ilivyokusudiwa katika AMV;

v. Tanzania ionyeshe kwa vitendo juhudi zile zile ilizozifanya kuhusu uanzishaji wa mfuko maalumu wa mapato ya gesi kwa madini mengine. Madini mengine pia yana umuhimu sana, na mantiki hiyo hiyo iliyotumika katika sekta ya gesi pia inaweza kutumika kwa hayo madini mengine na

vi. Pamoja na ushuru wa ndani, Tanzania inahitaji kuandaa mkakati wa kisera kuhakikisha kwamba jamii, ambazo zinaathirika na shughuli za uchimbaji madini kutokana na uchafuzi wa hali ya hewa na uharibifu wa mazingira, pia zijisikie kuwa ni sehemu ya miradi ya uchimbaji madini. Sehemu ya mapato yanayotokana na uchimbaji madini inaweza kuwekezwa tena katika jamii kwa kupitia miradi ya miundo mbinu inayokusudiwa kuboresha afya, elimu, maji na usafi wa mazingira.

Katika ngazi ya kanda, inapendekezwa kuwa kuna haja ya haraka ya kupatikana kwa mkakati wa uchimbaji madini ambao unakubalika na mataifa washirika. Pamoja na hayo, sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inaweza kutumia fursa inayotokana na Tanzania kukataa kutia sahihi Hati za Awali (protocol) za uchimbaji madini kwa kuandaa mkakati mpya unaoendana na AMV katika vipengele vyote, ikijumuisha mapato yanayotokana na madini na usimamizi wake. Uwepo wa AMV unasaidia, kwani unazungumzia masuala yenye manufaa kwa nchi zote, ambazo wanachama wameshakubaliana nazo.

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Februari 2009, Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika ulipitisha mfumo wa kukuza mpango wa maendeleo wa rasilimali za madini na mabadiliko ya kimuundo unaojulikana kama Dira ya Madini ya Afrika (AMV). AMV inataka kukuza utumiaji bora wa rasilimali ya madini unaozingatia uwazi na usawa kwa maendeleo mapana na endelevu kiuchumi na kijamii. Kichocheo hasa cha kupitisha AMV kilikuwa kuhakikisha kuwa kunakuwa na mabadiliko ya kifikra/mtazamo katika utawala wa rasilimali ya madini katika bara la Afrika, na mabadiliko haya yanayohusu madini kutumika kama mkakati kwa maendeleo kwa ujumla. Wasiwasi ulikuwa kwamba wakati nchi za Kiafrika zilikuwa zimetunukiwa rasilimali kubwa ya madini, manufaa yanayotokana na madini ni madogo sana, kwani mengi huuzwa nchi za nje kama malighafi, wakati ambapo mapato yanategemea mabadiliko katika bei za bidhaa kimataifa.

Mojawapo ya taratibu ambazo manufaa yanayotokana na rasilimali madini yanaweza kuhakikishwa chini ya AMV ni kuhakikisha kuwa uhusiano kati ya viwanda vya madini na sekta nyingine unaimarishwa. Hili litahitaji pia hatua za kuhakikisha kuwa mgawanyo wa mapato yanayotokana na sekta ya madini unafanyika kwa njia inayofaa. Kwa hiyo, mfumo wa utawala wa fedha pamoja na matumizi ya mapato yanayotokana na madini ni sehemu ya msisitizo wa AMV. Huu ni muktadha ambao kwayo utawala wa mfumo wa uchimbaji madini nchini Tanzania unatathminiwa katika utafiti huu.

AMV ilibuniwa ili kubaini hatua za baadaye za kuchukuliwa na nchi wanachama wa AU kuhusu sekta ya madini. Kwa hiyo, kuna haja ya kutathmini kiwango ambacho nchi wanachama wa AU zimefikia katika kuhakikisha kuwa zinaweka mikakati iliyobainishwa kuwa ya muhimu chini ya AMV. Hii itajumuisha kuainisha mapungufu kati ya yale yanayotakiwa kuwa katika AMV na hali ilivyo katika nchi (za kiafrika), jambo ambalo ni muhimu kwa sababu za kisera.

Ingawa AMV ina sehemu kuu saba, utafiti huu unalenga utawala wa fedha na usimamizi wa mapato tu. Katika eneo hili lililolengwa, utafiti unafanya tathmini ya Tanzania pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, ukilenga kwenye kubaini upungufu (mapengo) kati ya kile ambacho AMV inataka na hali halisi katika nchi.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

**Malengo makuu ya huu utafiti yalikuwa:**

i. Kuainisha usimamizi wa fedha katika sekta ya madini na masharti ya jinsi mapato yanayotokana na madini yanavyotumika na kusimamiwa Tanzania na katika nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
ii. Kutathmini upungufu kati ya hali ilivyo katika ngazi za taifa na kanda na za malengo ya AMV;
iii. Kutengeneza alama teule kupima upungufu kati ya utawala wa Tanzania na AMV kuhusiana na usimamizi wa fedha na mapato ya madini.

## 1.3 Mbinu za Utafiti

Taarifa kwa ujumla ni mapitio ya maandishi yaliyopo kuhusu AMV, katika sekta ya madini Tanzania, sera ya mapato na sheria ya sekta ya madini Tanzania, pamoja na usimamizi wa mapato ya sekta ya madini kwa ujumla. Mategemeo zaidi yaliwekwa katika makala rasmi za kiserikali na takwimu kutoka taasisi za umma zinazoshiriki katika viwanda vya madini Tanzania, ikiwa pamoja na Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Vifungu muhimu vya AMV, hasa vile vinavyohusu utawala wa fedha za sekta ya madini na usimamizi wa mapato yalitumika kama kigezo au alama teule (benchmark) hasa kama ilivyobainishwa chini ya 'Mpango wa Utekelezaji wa AMV' wa Desemba 2011. Uchaguzi wa alama teule ulihusu kuainisha shughuli, muda na viashiria vya ufuatiliaji ambavyo nchi zinapaswa kufuata na kuangalia kama hivyo vipo katika ngazi za kanda na za kitaifa.

Ingawa utafiti pia unajaribu kuainisha hatua zote zilizochukuliwa kama jibu kwa AMV, utafiti unajikita zaidi katika kuchambua upungufu uliyomo. Hii ni kwa sababu, ni vigumu kubaini moja kwa moja mabadiliko husika yametokana na nini; hatua za kisera zinaweza kupitishwa baada ya kuanzishwa kwa AMV lakini ikafanyika kutokana na sababu nyingine na siyo kwa sababu ya AMV. Kwa hiyo utafiti unajikita katika kuainisha upungufu kati ya vifungu vya AMV na hali halisi katika nchi. Kama hakuna upungufu uyobainishwa, hapo mfumo wa utawala unaonekana kuwa unaendana na vifungu vya AMV. Hii mbinu ilichaguliwa kutumika kwa kuwa lengo kuu la taarifa hii ni kuanisha maeneo ambayo bado yanahitaji kushughulikiwa katika muktadha wa AMV. Maeneo ambayo tayari yanafungamana na AMV hayahitaji kufanyiwa kazi zaidi, hata kama hayakuwa hivyo kutokana na AMV.

Utafiti pia haukujikita sana katika masuala ya uchumi wa kisiasa katika sekta ya madini kwa ujumla, ingawaje hii ingelieleza mwelekeo mkuu wa AMV. Hii inajumuisha masuala ya kisiasa na uchumi kama vile kutathmini kama shughuli za uchimbaji

madini kufanywa na wazawa,  soko huria, na ushiriki wa mataifa ya nje katika uchimbaji wa madini kunakuza maendeleo.

Utafiti pia ulitengeneza kadi ya alama (scorecard), ambayo inajaribu kupima, katika mizani inayoanzia sifuri hadi tano, kiwango ambacho mfumo wa utawala/usimamizi Tanzania kinafanana na vifungu vya AMV. Alama ya sifuri inaonyesha kwamba hakuna kiashiria chochote kinachofungamana na AMV wakati alama ya tano inaonyesha viashiria vyote vinafungamana na AMV. Kadi ya alama ilitengenezwa na waandishi na tunakubali kwamba huenda kukawa na kiwango fulani cha udhanifu (subjectivity) katika vipimo hivi. Lakini, utoaji alama ulitegemea jinsi kila kipimo kinavyotathminiwa katika utafiti, kwa hiyo waandishi wanaona  kuwa kulikuwa na kiwango fulani cha utaratibu unaozingatia uhalisi (objectivity).

# 2. MASHARTI MUHIMU YA AMV KUHUSU UTAWALA WA FEDHA NA USIMAMIZI WA MAPATO KATIKA SEKTA YA MADINI

Mojawapo ya mikakati iliyoainishwa na wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika na Serikali kuhakikisha utekelezaji wa ufanisi wa vifungu vya AMV ilikuwa kuanzishwa kwa Kituo cha Kiafrika cha Maendeleo ya Madini (AMDC) kutoa msaada wa kimkakati katika shughuli za utekelezaji wa dira na mpango wake. Novemba 2012, Mpango Kazi wa Kituo cha Kiafrika cha Maendeleo ya Madini (AMDC) uliandaliwa kwa msaada wa Serikali ya Australia na Serikali ya Canada. Dhima ya AMDC ni kufanya kazi pamoja na nchi wanachama wa AU na mashirika yao ya kitaifa na ya kikanda ikiwa ni pamoja na Kamisheni ya Umoja wa Kiafrika (AUC), Ushirika Mpya kwa Maendeleo ya Afrika (NEPAD), Shirika la Kitaifa la Mipango na Uratibu (NPCA), Jamii za Kiuchumi za Kanda (RECs) kuwezesha rasilimali ya madini kuleta mabadiliko zaidi katika maendeleo ya Bara la Afrika kupitia ongezeko la mahusiano ya kiuchumi na ya kijamii, na kwa jinsi hii kusaidia kushughulikia umaskini wake usio na mwelekeo na maendeleo yake finyu. Hata hivyo, ingawa AMDC sasa imeshaanzishwa, haijaweza kuwajibika kikamilifu katika kuhakikisha kuwa nchi nyingi zinaanza mchakato wa kuoanisha na kupanga kwa kina (mapping) AMV kwa nchi zao.

AMV inapanga matarajio yake katika vikundi vitatu: Yale ambayo ni ya muda mfupi (ndani ya miaka 5), yale ya muda wa kati (miaka 5-20) na ya muda mrefu (zaidi ya miaka 20). Masharti yanayohusu utawala wa fedha na usimamizi wa mapato wa sekta ya madini ni pamoja na yafuatayo:

### a. Masuala ya muda mfupi

Matarajio ya AMV ya muda mfupi yanajumuisha kukuza utawala wa rasilimali za maliasili. Hii ni pamoja na kusimamia ushiriki wa wadau[1] kwa muda wote wa hatua mbalimbali za mzunguko wa maisha ya mgodi[2] na kuboresha usimamizi wa uhawilishaji bei unaohusiana na shughuli za uchimbaji madini. Katika muktadha wa viwanda vya madini uhawilishaji huu wa malipo unajikita zaidi katika marejesho (returns) kwa wanahisa na watoa huduma katika hatua zote za mzunguko wa maisha ya mgodi. Ili kufanikisha hili, AMV inapendekeza shughuli zifuatazo:

i. Uingizaji wa kanuni za Mpango wa Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji (EITI) na Mpango wa Kimberly wa Mchakato wa Utoaji Vyeti katika sera za kitaifa, sheria na kanuni;
ii. Kuhimiza uanzishaji wa vyombo vya kitaifa vya usimamizi wa sheria/kanuni na kushirikisha wabunge na kamati huru katika ufuatiliaji wa miradi ya uchimbaji madini;
iii. Uzingatiaji wa ugatuzi wa madaraka ya ugawaji wa mapato yanayotokana na madini na
iv. Ujenzi wa uwezo wa taasisi za kitaifa na za chini yake kusimamia mapato yanayotokana na madini.

AMV pia inazingatia kukuza hali ya usawa baina ya vizazi katika kushirikiana rasilimali zinazotokana na sekta ya madini kama moja ya tarajio lake la muda mfupi. Kufikia mafanikio haya, AMV inapendekeza kwamba nchi zizingatie uanzishaji wa "Mifuko ya Kizazi cha Baadaye" na 'Mifuko ya Udhibiti' kama mikakati ya kujenga rasilimali ambazo zitanufaisha vizazi vijavyo. AMV pia inapendekeza uingizaji wa uchimbaji madini katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa na Mkakati wa Kupunguza Umaskini kama mkakati wa kuhakikisha usawa kati ya vizazi. Lengo pia linaweza kufikiwa kwa kuzingatia mipango ya kugatua madaraka ya usambazaji wa mapato na ugawaji wake pamoja na kuhakikisha ushiriki mpana na unaoonekana wa jamii zinazohusika na miradi ya madini katika uidhinishaji, upangaji, utekelezaji, na ufuatiliaji wa miradi ya uchimbaji madini. Tarajio lingine la muda mfupi la AMV ni kwa nchi kuhakikisha ukusanyaji wa mitaji katika sekta ya madini. Hii ni pamoja na kuleta pamoja nguvu zilizofichika za ushirika wa sekta za umma na za binafsi pia kubuni mbinu za kuboresha akiba ya ndani na kuielekeza katika kugharamia miradi / mipango ya taifa.

### b. Masuala ya muda wa kati

Katika muda wa kati, AMV inapendekeza nchi ziimarishe utekelezaji wa viwango, sheria au kanuni zinazotawala tasnia ya madini. Hii itahusu uimarishaji wa mfumo wa sheria na kanuni zinazotawala uchimbaji madini na kuongeza uelewa wa umma na ushiriki wao katika kuandaa mfumo wa kanuni hizo. Hii pia inajumuisha maandalizi ya mikakati ya kuhakikisha ufuataji wa sheria zilizowekwa, yenye idhini ya kutoa adhabu na kunyanganya leseni pale ambapo kuna uvunjaji wa sheria kuhusu rasilimali za madini. Sheria zinazotawala tasnia ya madini pia zinahitaji kuwa thabiti na zenye kutabirika kwa kuandaa kanuni zilizo wazi na miongozo ili kupunguza uwezekano wa sheria kutotafsiriwa vizuri.

---

[1] Kuna aina mbalimbali za wadau wanaoweza kubainishwa kwa muda wote wa hatua mbalimbali za mzunguko wa maisha ya mgodi. Hii inajumuisha jamii iliyoathirika kutokana na uchimbaji, kampuni za uziduaji, mafundi wachundo na wachimbaji wadogo, washauri wa sekta ya madini, wanasheria, wafadhili, wachunguzi, wachambuaji, makampuni ya ufungaji wa vyuma na uchimbaji, makampuni ya usafirishaji, serikali na mashirika ya umma, pamoja na wabobezi wengine wanaoshughulika na ufikiaji ukomo na shughuli za usafishaji wa mazingira.

AMV pia inapendekeza hitaji la kuimarisha mnyororo wa thamani na kuongeza utofauti wa uchumi kama sehemu ya matarajio yake ya muda wa kati. Hii itajumuisha kutengeneza na/au kuuza bidhaa za aina nyingine badala ya rasilimali ya madini jambo ambalo litajumuisha pia upatikanaji wa mazingira mazuri kwa maendeleo ya mahusiano madhubuti baina ya sekta ya madini na sekta zengine (forward and backward linkages), ongezeko la thamani hasa uchakataji wa mwanzo na uundaji wa vikundi pamoja na ushirikiano wa teknolojia miongoni mwa nchi. Hii pia itajumuisha uwekezaji wa mitaji iliyopatikana kutokana na rasilimali katika sekta nyingine za uchumi.

**c. Muda mrefu**

Kuhusu tasnia ya madini, matarajio ya muda mrefu ya AMV ni ongezeko kubwa (hadi upeo) la wawekezaji wa kiuchumi na mfuriko (yaani, ongezeko la maendeleo ya kiuchumi kwa kuwa fedha za madini zinaweza kuchochea maendeleo ya sekta nyingine pia jamii inaweza kunufaika moja kwa moja kutokana na maendeleo ya sekta ya madini). Hii itafanikiwa kwa kuwa na bidhaa za sekta nyingine yaani kutokutegemea rasilimali za madini peke yake, kutokana na kuhakikisha kuwa mitaji inayopatikana kutoka sekta ya madini inawekezwa katika sekta nyingine za uchumi. Kwa hiyo matarajio ya muda mrefu yanahusisha zaidi ukusanyaji pamoja wa mafanikio yanayotokana na tasnia ya madini na kuhakikisha kuwa madini yanachangia kwa kiasi cha kuridhisha katika pato la taifa (zao ghafi la ndani) pamoja na kupunguza umaskini na kuboresha hali ya maisha ya jamii.

## 2.1. Mpango wa Utekelezaji wa AMV, 2011

Mwezi Februari 2009, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika waliwaagiza mawaziri wanaosimamia maendeleo ya rasilimali ya madini kutengeneza mpango halisi wa utekelezaji ili kufikia malengo ya AMV. Matokeo ya agizo hili yakawa kuandaliwa kwa 'Mpango wa Utekelezaji wa AMV' Desemba 2011, ambao ulikuwa na vifungu tisa vya mipango ya shughuli, yaani: kodi ya madini (pato litokanalo na umilikaji wa ardhi) na usimamizi wake; mifumo ya kijiolojia na uundwaji wa madini; ujenzi wa uwezo wa watu na taasisi; mafundi uchundo na wachimbaji wadogo wadogo; udhibiti katika sekta ya madini; utafiti na maendeleo; mazingira na masuala ya kijamii; uhusiano na ubadilishaji biashara / bidhaa na uhamasishaji wa uwekezaji katika uchimbaji madini na miundo mbinu.

Kwa hiyo, mpango wa Utekelezaji wa AMV unaweza kutumika kama kipimo katika kutathmini ni kwa kiwango gani nchi zimeoanisha na kupanga kwa kina mikakati ya AMV katika sera zao za sekta ya uchimbaji madini. Kuhusu udhibiti wa fedha na usimamizi wa mapato katika sekta ya madini, ifuatayo ni mipango halisi iliyokubaliwa katika muda mfupi (ST), muda wa kati (MT) na muda mrefu (LT) kwa ngazi ya taifa (Jedwali 1):

[2] Mzunguko wa maisha ya mgodi una hatua tano: (1) majadiliano ya mikataba na sahihi; (2) shughuli za uchunguzi na tathmini; (3) ujenzi wa miundo mbinu; (4) uziduaji, uzalishaji na mauzo nje ya nchi; pamoja na (5) kuacha na kufikia ukomo

**Jedwali 1: Mikakati ya Utawala wa Fedha na Usimamizi wa Mapato kwa Sekta ya Madini chini ya AMV kwa Ngazi ya Taifa**

| Matokeo tarajiwa | Shughuli | Muda | Viashiria vya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|
| Ongezeko la mgawo wa mapato yanayotokana na madini kwa nchi za Kiafrika zenye madini | Imarisha uwezo wa kitaifa kufanya ukaguzi halisi wa uzalishaji madini na mauzo nje ya nchi halisi ki-vitendo | ST | Mfumo wa ukaguzi kivitendo upo na unatekelezwa na wakaguzi waliofunzwa |
| | Fanya mapitio ya utawala wa madini kwa lengo la kuongeza mapato hadi upeo wa juu kabisa. | ST | Mapitio ya usimamizi wa madini yamefanyika na kiwango cha uboreshaji katika mapato ya fedha zilizokusanywa na nchi za Kiafrika zenye machimbo ya madini. |
| | Jenga uwezo na ongeza stadi za maofisa katika kujadili masuala ya fedha na kufuatilia kwa ufanisi ufuataji na utekelezaji wa sheria za kodi. | ST-MT-LT | Ongezeko katika idadi ya watunga sera na wadau wengine wanaoshiriki katika shughuli za ujenzi wa uwezo. |
| | Jadili au jadili tena mikataba ili kuongeza mapato na kuhakikisha uwepo wa fedha na uwezo wa kujikimu endapo kuna dharura. | ST-MT | Kiwango cha uboreshaji katika uandishi wa masharti ya kifedha. |
| | Unda mifumo ya kutathmini vipengele vya udhibiti wa kodi kwa kuchunguza uvujaji, upotevu na ukwepaji na uepukaji kodi (k.m. uhawilishaji bei). | ST-MT | Kiwango cha upunguzaji wa uvujaji wa kodi kwa kutumia mifumo ya tathmini kama ilivyoainishwa na kaguzi huru za udhibiti wa kodi (ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni za kodi). |
| | Kurejea masharti ya mikataba ya tozo la kodi maradufu na BITs pamoja na nchi wenyeji wa makampuni ya uchimbaji madini ikijumuisha kanuni ya madini kutozwa kodi katika hatua ya uziduaji. | ST-MT- | Idadi ya mikataba ya utozaji kodi mara mbili iliyowekewa sahihi na inayotekelezwa na nchi wanachama. |
| | Jenga uwezo na mifumo ya kunadi haki za madini pale inapowezekana. | ST | Kiwango cha utekelezaji wa mifumo ya umiliki madini ulio na ushindani na uwazi. |
| Kuboreshwa kwa usimamizi na matumizi ya mapato yanayotokana na madini | Chunguza mikakati ya kuwekeza mapato yasiyotegemewa, mapato ya kawaida na kodi ya madini katika mifuko huru ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na mfuko wa udhibiti na mfuko wa miundo mbinu. | ST | Idadi ya SWFs zilizoanzishwa na nchi za Afrika zenye madini. |
| | Andaa mifumo ya kusambaza kodi ili kugawa sehemu ya mapato yanayotokana na madini kwa jamii na mamlaka za jamii zinazoishi jirani na migodi. | ST | Kiwango ambacho mamlaka ya Serikali za Mitaa na jamii wananufaika kutokana na miradi ya uchimbaji madini. |
| | Andaa mipango ya kuwezesha jamii husika kupata kazi, elimu, miundo mbinu ya usafiri, huduma za afya, maji na usafi wa mazingira. | ST-MT | Kiwango ambacho mamlaka ya Serikali za Mitaa na jamii wananufaika kutokana na miradi ya uchimbaji madini. |
| | Jenga uwezo wa jamii kujadili mikataba ya ushirikiano. | MT | Kiwango ambacho mamlaka ya Serikali za Mitaa na jamii wanaboresha usimamizi wa mapato yanayotokana na madini. |
| | Kuza mifumo ya kuimarisha uwezo wa vyombo vya ngazi ya kitaifa na vya chini yake kusimamia mapato. | MT | Kiwango ambacho miongozo inatumiwa na RECs na nchi wanachama |

*Chanzo: Mpango wa Utekelezaji wa AMV, 2011.*

Mpango wa utekelezaji pia unaainisha mikakati na viashiria vya ufuatiliaji katika ngazi ya kanda (jedwali 2) ambao pia una muda wa utekelezaji uliowekwa wazi.

**Jedwali 2: Mikakati ya Utawala wa Fedha na Usimamizi wa Mapato kwa Sekta ya Madini chini ya AMV kwa Ngazi ya Kanda**

| Matokeo Tarajiwa | Shughuli | Muda | Viashiria vya Ufuatiliaji |
|---|---|---|---|
| Ongezeko la mgawo wa mapato yanayotokana na madini kwa nchi za Afrika za uchimbaji madini. | Fanya mapitio ya mazingira ya kifedha ya sasa katika nchi za uchimbaji madini za Afrika ili kuandaa miongozo na viwango vya kuboresha mifumo ya mapato (k.m. kodi na gawio) katika njia ambazo hazitakatisha tamaa wawekezaji wa uchimbaji madini. | ST- | Miongozo, viwango na zana zinazohitajika zimekamilika na zimesambazwa kwa RECs na nchi wanachama. |
| | Andaa miongozo ya utozaji kodi za madini kwa utekelezaji katika ngazi ya REC & na Taifa. | ST- | Miongozo, viwango na zana zinazohitajika zimekamilika na zimesambazwa kwa RECs na nchi wanachama. |
| | Andaa mifano (modeli) ya mifumo ya kawaida ya usimamizi wa fedha kwa miradi ya madini kwa ajili ya nchi wanachama na endesha warsha za mafunzo katika ngazi ya REC. | ST- | Idadi ya modeli za usimamizi wa fedha ambazo zimeandaliwa na kutumiwa na nchi wanachama. |
| Kuboreshwa kwa usimamizi na matumizi ya mapato yanayotokana na madini. | Kusanya miongozo bora iliyohakikiwa kuhusu usimamizi wa mapato yanayotokana na madini na usambazaji wake kwa REC na ngazi ya Taifa kwa ajili utekelezaji. | | Miongozo iliyohakikiwa kuhusu usimamizi wa mapato ya madini imekusanywa. |

*Chanzo: Mpango wa Utekelezaji wa AMV, 2011.*

Huu kwa ujumla ndio muktadha ambao kwamo tathmini itafanyika. Madhumuni ya taarifa hii ni kutathmini ni kwa kiwango gani mfumo wa udhibiti wa fedha na usimamizi wa matumizi ya mapato kwa sekta ya sasa ya madini inarandana / fungamana na matarajio ya AMV.

# 3. MAELEZO YA JUMLA YA SEKTA YA MADINI TANZANIA

Tanzania imetunukiwa aina mbalimbali za akiba ya madini ardhini na inatambulika kama mojawapo ya nchi za kiafrika zilizo na utajiri wa rasilimali hii. Madini yanayopatikana Tanzania yanaweza kugawanywa katika makundi ya aina tano: madini ya chuma, mawe ya thamani (gemstones), madini ya viwandani, vifaa vya ujenzi, na madini ya nishati. Mifano ya madini kutoka kila kifungu yanaonekana katika kisanduku cha 1. Tanzania pia ina madini mengi ambayo bado hayajachimbwa kwa kuwa uchunguzi mwingi bado unaendelea, kuna uwezekano wa ongezeko zaidi la mchango wa sekta hii.

**Kisanduku 1: Mifano ya madini yanayopatikana Tanzania**

**Madini ya Metali**

- Dhahabu, chuma, shaba, fedha, platinamu, nikeli na bati (tin);

**Vito vya Mapambo (Gemstones)**

- Almasi, tanzanite, rubi (ruby), ganeti, emerald, alexandrite na johari (sapphire);

**Madini ya Viwandani**

- Kauri (kaolin), fosfati (phosphate), lime, jasi (gypsum), diatomite, bentonite, vermiculite, chumvi na mchanga wa ufukweni;

**Vifaa vya Ujenzi**

- Mawe mchanganyiko na mchanga na

**Madini ya Nishati**

- Mkaa wa mawe na urani (uranium)

Hii akiba ya madini inaweza kupatikana sehemu zote za nchi, ingawa kuna sehemu fulani za nchi zinajulikana tangu asili kuwa na aina fulani za madini. Kwa mfano, dhahabu hupatikana katika ukanda wa mawe ya kijani (greenstone belt) kusini, mashariki na magharibi mwa Ziwa Victoria wakati almasi inapatikana katika mabomba ya kimberliti ya kati na kusini mwa Tanzania na sehemu ya kusini mwa Ziwa Victoria kwenye eneo ambapo dhahabu inapatikana. Madini ya nikeli, cobalt, shaba, bati (tin), na tungsten yanapatikana zaidi kaskazini-magharibi mwa Tanzania wakati titanium, vanadium na chuma ziko zaidi kusini – magharibi ya Tanzania. Hali kadhalika, makaa ya mawe yanapatikana zaidi kusini – magharibi mwa Tanzania wakati uranium inapatikana katikati na kusini mwa Tanzania. Magadi, chumvi, jasi (gypsum), travertine na trona (vivukizo) yanapatikana zaidi katika bonde la ufa na ukanda wa pwani, wakati madini ya kaolin, mica, phosphate, magnesite, mchanga wa ufukweni, diatomite, mawe mchanganyiko, mawe ya kipimo cha aina yoyote (dimension stone), na mchanga yanaweza kupatikana sehemu mbali mbali za Tanzania.

Ingawa sekta ya uchimbaji madini ni muhimu Tanzania, mchango wake kwa Pato laTaifa (GDP) ni mdogo ukilinganisha na sekta nyingine za uchumi. Kwa mfano, kati ya 2007 na 2012, wastani wa mchango unaotokana na uchimbaji madini na uchimbaji/uvunjaji mawe ulikuwa 2.8% wakati sekta nyingine kama kilimo na uvuvi ulikuwa (24%), ujenzi na viwanja (17.2%), biashara, hoteli na migahawa (17%); bidhaa za viwandani (9%) na usafiri & mawasiliano (8%) zilifanya vizuri zaidi (Baunsgaard, 2014). Mchango wa sekta ya uchimbaji madini kwenye Pato la Taifa (zao ghafi la ndani) uliongezeka hatua kwa hatua kutoka 1.4% mwaka 1998 hadi 3% mwaka 2008, lakini kadiri sekta nyingine zilivyoongeza uzalishaji mchango wake ukapungua hadi 2.5% mwaka 2009 na 2.4% mwaka 2010 (Muganyizi, 2012). Kwa sasa, mchango wa sekta ya madini kwa GDP unakadiriwa kuwa 3.5%, ingawa mchango huu unategemewa kufikia 10% GDP ifikapo 2025 kutokana na taratibu mbalimbali ambazo zimeanzishwa katika sekta ya madini (Wizara ya Nishati na Madini (MoEM), 2015).

Mtazamo kwenye ujazo wa uzalishaji wa madini makuu kutoka migodi mikubwa unaonyesha kwamba kumekuwa na mwelekeo wa ujumla wa kwenda juu (ongezeko) katika ujazo wa madini yaliyozalishwa tangu 1999 (Chati1). Uzalishaji wa dhahabu uliongezeka toka karibia tola wakia tani 130 elfu mwaka 1999 hadi tola wakia milioni 1.27 mwaka 2014. Fedha nayo pia iliongezeka toka karibu tola wakia elfu 10 mwaka 1999 hadi wakia 470 elfu mwaka 2014. Shaba iliongezeka toka paundi milioni 5.73 mwaka 2001 hadi paundi milioni 13.78 mwaka 2014. Almasi, lakini, haikufanikiwa kuwa na mweleko wa juu kama mwaka 2014 iliendelea kuwa na ujazo wake wa karibu karati 230 elfu kama ilivopimwa mwaka 1999.

Kumekuwa na mabadiliko mengi katika ujazo wa madini, ambayo yanaathiriwa na muda wa maisha ya miradi pamoja na muundo wa migodi yenyewe, ambapo nyakati fulani kiasi cha madini yanayochimbwa huwa kidogo.

**Chati 1: Historia ya Mauzo ya Madini Kutoka Migodi Mikubwa (1999-2014)**




***Chanzo:*** *Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA), 2014.*

Sekta ya madini ni muhimu pia kama chanzo cha mapato ya kodi kwa Serikali. Mchango wa mapato toka sekta ya madini kutoka migodi mikubwa tisa kwa jumla ya mapato uliongezeka toka 2.41% mwaka 2001 hadi 4.41% mwaka 2014, ingawa ilifikia kiwango cha juu kabisa cha 10.97% mwaka 2012 (Jedwali 3). Kwa hiyo kwa wastani, migodi tisa mikubwa imechangia 4% ya jumla ya mapato yote ya kodi kwa uchumi wa Tanzania bara.

**Jedwali 3: Mchango wa migodi tisa ya madini katika jumla ya mapato ya kodi Tanzania Bara**

| | Mrabaha (royalty) | Kodi zingine | Jumla ya kodi zilizolipwa | Jumla ya mapato ya kodi | Kodi ya madini/Jumla ya mapato ya kodi (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2001 | 6.56 | 13.57 | 20.13 | 834.764 | 2.41 |
| 2002 | 10.22 | 19.41 | 29.63 | 941.5965 | 3.15 |
| 2003 | 14.97 | 22.09 | 37.06 | 1107.954 | 3.34 |
| 2004 | 18.87 | 20.95 | 39.82 | 1339.195 | 2.97 |
| 2005 | 21.34 | 37.16 | 58.5 | 1625.239 | 3.60 |
| 2006 | 29.3 | 22.21 | 51.51 | 1968.593 | 2.62 |
| 2007 | 30 | 34.18 | 64.18 | 2575.649 | 2.49 |
| 2008 | 32.69 | 67.27 | 99.96 | 3376.568 | 2.96 |
| 2009 | 43.34 | 82.16 | 125.5 | 4051.964 | 3.10 |
| 2010 | 70.37 | 100.63 | 171 | 4437.933 | 3.85 |
| 2011 | 97.03 | 208.68 | 305.71 | 5315.148 | 5.75 |
| 2012 | 115.17 | 597.88 | 713.05 | 6502.6 | 10.97 |
| 2013 | 112.42 | 215.03 | 327.45 | 7739.298 | 4.23 |
| 2014 | 102.88 | 311.32 | 414.2 | 9383.047 | 4.41 |

***Chanzo:*** *TMAA, 2014 na Mamlaka ya Mapato Tanzania Kanzi Data ya Takwimu za Taifa*

Sekta ya madini ilipanuka kwa haraka baada ya mabadiliko ya sera ya madini ya mwaka 1997, ambapo ilishuhudiwa wadau wengi wakiingia kwenye sekta. Kuna kama migodi 8 mikubwa (sita ya dhahabu na miwili ya vito vya mapambo (gemstone)) na migodi mingine midogo mingi ambayo mingi ni ya dhahabu, almasi na madini ya vito. Idadi fulani ya miradi ya uchimbaji iko katika hatua za juu, nayo inategemewa kukua na kuzalisha kwa kiwango cha juu. Mifano ya miradi ya jinsi hiyo inaonekana katika Kisanduku 2.

**Kisanduku 2: Miradi ambayo sasa iko katika hatua za juu za uchunguzi**

| | | |
|---|---|---|
| Kabanga nickel project | Mantra uranium project | Mchuchuma coal project |
| Liganga iron ore project | Nyanzaga gold project | Canaco gold project |
| Panda Hill niobium project | Ngualla REEs project | Resolute-Nyakafuru gold project |
| Uranex graphite project | Dutwa nickel project | Ngwena nickel project |
| Kiwira coal project | | |

*Chanzo: MoEM, 2015*

Mabadiliko mbalimbali yaliyofanyika katika sekta ya madini yanaweza kuwa sababu ya maendeleo mazuri yaliyoshuhudiwa katika sekta. Mapato yanayotokana na mauzo ya nje yaliongezeka kutoka wastani wa 1% ya jumla ya mauzo ya nje mwaka 1997 hadi 52% mwaka 2013; ajira ya moja kwa moja katika viwanda vikubwa vya uchimbaji madini iliongezeka toka 1,700 hadi 15,000 mwaka 2013 (MoEM, 2015).

Utendaji wa sekta ya madini unatokana na mabadiliko mbalimbali ya kisera yaliyofanywa na Serikali kwa kipindi cha miaka kadhaa. Haya ni pamoja na utayarishaji wa sera ya madini ya mwaka 2009, uwekwaji wa sheria ya uchimbaji madini ya mwaka 2010 (ambayo iliondoa na kuwa badala ya sheria ya uchimbaji madini ya mwaka 1979 na sheria ya uchimbaji madini ya mwaka 1998) na uanzishaji wa motisha ya kifedha iliyolenga katika kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi. Sera ya madini ya mwaka 2009 ilitungwa kama sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025. Malengo ya sera ya madini yanajumuisha:

I. Kuendelea kuvutia wawekezaji binafsi katika uchunguzi na uchimbaji madini;
II. Serikali ishiriki katika miradi ya ki-mkakati;
III. Kusisitiza muunganiko wa sekta ya madini na uchumi kwa ujumla;
IV. Kuanzisha utawala wa fedha unaoleta usawa baina ya manufaa na ushindani wa uwekezaji;
V. Kusaidia manufaa yanayotokana na madini na upatikanaji wa masoko;
VI. Kusisitiza maendeleo ya wachimbaji wadogo;
VII. Kuimarisha ushiriki wa umma katika shughuli za uchimbaji madini;
VIII. Kuwaongoza wawekezaji katika uchimbaji endelevu wa rasilimali ya madini nchini Tanzania katika njia ambayo pande zote wananufaika.

Baada ya mabadiliko haya, uzalishaji mkubwa wa dhahabu hufanywa zaidi na migodi saba. Mgodi wa Bulyanhulu Gold Mine Ltd ulianza uzalishaji mwaka 2001. Mgodi wa North Mara Gold Ltd ni mgodi mwingine wa dhahabu, ambao ulianza uzalishaji mwaka 2002 chini ya umiliki wa mgodi wa Afrika Mashariki Gold Mines Ltd. Migodi mingine mikubwa ni pamoja na Mgodi wa Dhahabu Tulawaka, Mgodi wa Dhahabu Geita, Mgodi wa Dhabu wa Golden Pride, Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba, na Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi.

Sera ya Madini ya Mwaka 2009 yaweza kuwa chanzo cha uboreshaji wa utendaji kutokana na sababu mbalimbali. Sera hii ilianzishwa kuwa mbadala wa Sera ya Madini ya 1997, ambayo ilikuwa na udhaifu fulani. Kwa mfano, hivi sasa msisitizo umewekwa katika kuhimiza muunganiko wa kiuchumi kati ya sekta ya madini na uchumi mkuu kwa ujumla kupitia shughuli za ongezeko la thamani pamoja na kuongeza kiasi cha mapato ambayo Serikali hupokea kutoka katika sekta, (Oxford Policy Management, 2011). Kwa hiyo, Sheria ya Madini ya 2010, ilibidi itungwe ili kuakisi huu mwelekeo mpya, kwani Sheria ya Madini ya mwaka 1998 nayo ilikuwa imetungwa kutegemeana na sera ya iliyokuwepo kabla ya hii ya sasa. Inahakikisha: usalama wa wawekezaji kwa muda wote wanapokuwa katika shughuli za madini; urejeshaji wa mitaji na faida kwao, na uwazi katika utoaji na usimamizi wa haki za madini.

**Chini ya Sheria ya Uchimbaji Madini ya mwaka 2010:**

i. Mmiliki wa rasilimali ya madini ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
ii. Shughuli zozote za uchunguzi au uchimbaji haziruhusiwi bila kuwa na Hati ya Haki ya Madini;
iii. Uwekezaji wa pamoja (joint ventures) na makampuni ya ndani ya nchi unasisitizwa;
iv. Uchunguzi na uchimbaji madini ni wazi kwa wazawa na wageni au uwekezaji wa pamoja wa makampuni ya wazawa/wageni isipokuwa kwa yafuatayo:
    a) Wageni hawaruhusiwi kuwa na au kufanya uchunguzi / shughuli za uchimbaji kwa kutumia PMLs;
    b) Uchunguzi wa mawe ya thamani (gemstone) na uchimbaji wake unaruhusiwa kwa wazawa tu.

c) Biashara ya madini inaweza kuendeshwa na wazawa au kwa pamoja na wageni ambapo wazawa lazima wamiliki hisa zisizopungua 25% ya hisa za pamoja na
d) Utoaji leseni kwa ajili ya uchunguzi utafanyika kwa misingi ya kwamba anayekuja kwanza ndiye atakeyehudumiwa kwanza.

Sambamba na hitaji la kupata mapato zaidi, katika Sheria ya Madini ya 2010 mrabaha uliolipwa na makampuni ulibadilishwa kwa kutumia njia tofauti ya ukokotoaji pia kwa kiwango kilichotumika. Mirabaha sasa inakokotolewa kutegemea thamani ya jumla ya madini (wakati wa kuuza nje au pale mzigo unapofikishwa ndani ya nchi kuliko kutegemea thamani baada ya kuondoa gharama mbali mbali, mtindo uliokuwa ukitumika zamani. Wakati Rabaha unaotozwa kwa almasi umebakia kuwa 5% viwango kwa madini mengine viliongezeka (Oxford Policy Management, 2011).

Ili kufanya kazi katika tasnia ya uchimbaji madini, leseni ya biashara inahitajika na wanaweza kupatiwa wananchi wa Tanzania na wageni. Kwa nyongeza, leseni ya dalali ambayo hutolewa kwa wananchi wa Tanzania tu pia inahitajika. Leseni za biashara na za udalali zinaweza kutolewa kwa biashara zinazohusu dhahabu, madini ya chuma, vito vya mapambo, almasi, makaa ya mawe na madini ya viwandani.

Mfumo wa Tanzania wa utoaji leseni pia unatofautisha haki ya madini kwa kigezo cha kiwango cha uchimbaji na aina ya madini. Aina za madini chini ya Sheria ya Uchimbaji Madini ya 2010, zimeshajadiliwa kwenye Kisanduku 1. Aina za haki za madini chini ya Sheria ya Uchimbaji Madini ya 2010 zinajumuisha leseni ya utafutaji madini, leseni ya kubaki na haki ya kuchimba madini, leseni maalum ya uchimbaji, leseni ya uchimbaji, leseni ya uchakataji, leseni ya uchenjuaji na leseni ya usafishaji. Leseni ya utafutaji madini hutolewa kwa kipindi cha miaka mitatu na katika kila uombaji mpya, angalau 50% ya eneo huachiliwa.

Leseni ya uchimbaji madini hutolewa kwa watendaji wa kiwango cha kati ambao mtaji wa uwekezaji ni kati ya US$ milioni 100,000 na US$ milioni 100. Leseni maalum ya uchimbaji hutolewa kwa viwango vikubwa vya uchimbaji ambao mtaji wa uwekezaji siyo chini ya US$ milioni 100. Kwa kawaida, leseni ya kuchimba mawe ya thamani hutolewa kwa Watanzania, isipokuwa pale ambapo ujuzi, teknolojia au kiasi kikubwa cha mtaji kinahitajika kupata mali ghafi. Lakini, ushiriki wa mwekezaji mgeni sharti uwe chini ya 50% (MoEM, 2015).

**Ada ya maombi ya leseni kwa leseni mbalimbali ni kama ifuatavyo:**
i. Leseni ya utafutaji madini kwa madini ya chuma, madini ya nishati, madini ya vifaa vya ujenzi, mawe ya thamani na almasi ya aina ya kimberliti ni US$ 300;
ii. Leseni ya utafutaji kwa madini ya viwandani ni US$ 200;
iii. Leseni ya kubaki na haki ya kuchimba madini (retention) hugharimu US$ 4,000;
iv. Leseni maalum ya uchimbaji ni US$ 5,000;
v. Leseni ya uchimbaji ni US$ 2000.

Tanzania pia ina gharama za juu kwa leseni za biashara hasa kwa zile ambazo zinahusu dhahabu, almasi na madini mengine ya aina ya chuma. Leseni ya biashara kwa dhahabu, madini ya chuma na ya vito vyenye rangi hugharimu US$1, 000, ambazo hulipwa wakati wa upelekaji wa maombi kwa mara ya kwanza, wakati wa kuomba upya leseni kwa mara nyinge mfanya biashara atahitajika kulipa US$800. Leseni ya biashara kwa almasi US$2,000, wakati wa kuomba upya leseni kwa mara nyingine itagharimu $1,500. Leseni ya madini mengine hugharimu kidogo zaidi, kwa mfano, leseni ya mfanyabiashara wa makaa ya mawe na madini ya viwandani hugharimu kama US$500. Serikali, hata hivyo, huhakikisha kwamba biashara ya madini inahusisha ulipaji wa ada ambazo ni kubwa, ili kuhakikisha kwamba ni wale wawekezaji ambao wamejizatiti na wana nia ya dhati wanashiriki katika uchimbaji. Hii pia huwezesha kiasi kikubwa cha fedha kukusanywa kama mapato ya Serikali

Katika kufanya makazi kwenye ardhi kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini, Serikali ya Tanzania imepanga kodi inayotakiwa kulipwa kila mwaka kama “Eneo la Leseni” ambayo hulipwa kwa kila kilomita mraba. Kwa madini ya aina ya chuma, madini ya nishati, na madini ya almasi ya aina ya kimberliti, vifaa vya ujenzi na madini ya vito, kodi kwa mwaka kwa mara ya kwanza kwa leseni ya kutafuta madini ni US$ 150 kwa kilomita mraba moja, wakati kodi kwa mwaka kwa mara ya pili ni US$200 kwa kilomita mraba moja. Kodi ya mwaka inayotakiwa kulipwa na mwenye leseni maalum ya uchimbaji ni US$ 5,000 kwa kilomita mraba moja, wakati mwenye leseni ya uchimbaji kwa ajili ya madini ya aina ya chuma, ya nishati, vito na almasi ya aina ya kimberliti atatakiwa kulipa US$ 3,000 kwa kila kilomita mraba. Kulipia gharama kulingana na eneo la uchimbaji ni maendeleo mazuri kwani ni njia mojawapo ya fidia kwa kutumia ardhi. Ada ya maombi kwa kibali cha kuuza madini nje ya nchi ni US$ 100, wakati ada ya maombi ya kibali maalum kwa kuuza madini kwa wageni toka nje ni US$ 2,000. Ada ya maombi kwa kibali maalum cha kuuza madini yaliyonunuliwa katika tamasha la biashara la madini/vito ni US$ 200.

# 4. MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UTAWALA WA FEDHA KWA SEKTA YA MADINI TANZANIA

Sheria ya Uchimbaji Madini ya 2010 inatoa msingi kwa usimamizi wa fedha kwa sekta ya madini Tanzania. Pamoja na Sheria ya Uchimbaji Madini ya mwaka, 2010, sheria muhimu kwa sekta ya madini ni Sheria ya Kodi ya Mapato Kifungu 332 Toleo Lililopitiwa 2008 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya 2014. Hizi pamoja, na kanuni mbalimbali zinazopitishwa kila mwaka kuitikia matamko mbalimbali ya kisera ambayo yalielekezwa na tamko la bajeti la wakati husika, zimewezesha udhibiti wa fedha kwa sekta ya madini ambayo inatolewa maelezo kama ifuatayo:

## 4.1 Mirabaha

Wizara ya Nishati na Madini ina wajibu wa kuandaa sera na kuhakikisha kuwa inatekelezwa katika sekta nchini Tanzania. Pia ina wajibu wa kubainisha Mirabaha inayotakiwa ilipwe na mchimbaji, kwa kushauriana na Wizara ya Fedha. Kwa mujibu wa kifungu cha 87 hadi 92 cha Sheria ya Uchimbaji Madini ya 2010, kila mchimbaji mwenye kibali lazima alipe kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mrabaha kwa jumla yote ya madini yaliyozalishwa[3] kwa viwango vifuatavyo:

| Madini | Kiwango |
|---|---|
| Kwa upande wa urani | 5% |
| Vito (Gemstone) na almasi | 5% |
| Madini ya aina ya chuma kama vile: shaba, dhahabu, fedha, na madini ya kundi la platinam | 4% |
| Vito (Vilivyokatwa na kung'arishwa) | 1% |
| Dhahabu na madini mengine ya aina ya chuma | 4% |
| Madini, ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi, chumvi, na madini yote katika kifungu cha madini ya viwandani | 3% |

Hata hivyo, sheria inatamka kuwa kutakuwa na ada ya kuchambua bidhaa ambayo italipwa kwa Serikali na kila mwenye haki ya madini anayeamua kuuza vito vilivyozalishwa au alivyopata yeye kwenye kampuni inayomilikiwa na huyo mwenye haki ya madini.

## 4.2 Kodi ya Pembejeo

Kama sehemu ya motisha ya uwekezaji katika sekta ya uchimbaji madini, kampuni za uchimbaji hupewa misamaha kwenye ushuru wa uingizaji wa vifaa vya uchimbaji madini na bidhaa zinazotumika moja kwa moja katika shughuli za uchimbaji madini ambapo hupewa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kuanza uzalishaji. Baada ya shughuli zao, makampuni hupewa kikomo cha juu cha 5% cha ushuru wa bandari kwa uingizaji wa vifaa, mtaji na bidhaa. Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa mauzo ya ndani ni 18% na mauzo ya nje ni sifuri yaani hakuna kodi ya ongezeko la thamani. VAT iliyolipwa inaweza kurudishwa yote na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) hailipwi kwa huduma au bidhaa zinazotumika kwa shughuli za uchimbaji madini pekee. Wamiliki wa haki za madini pia wanapata msamaha wa kodi ya ndani ya zuio kwa bidhaa na huduma zinazotolewa na makampuni hayo. Lakini, watatakiwa kulipa kodi ya zuio kwa manunuzi wanayofanya wao kwa bidhaa au huduma za ndani ya nchi.

Kodi ya zuio kwa huduma za kiteknolojia kwa makandarasi wadogo ni 5% ya malipo ya jumla kwa wakazi (wananchi) na 15% ya malipo ya jumla kwa wasio wakazi (wageni toka nje) kwa kutegemea kiasi kilichopo kwenye hati ya madai. Kodi ya mafuta (Ushuru wa mafuta na forodha) inalipwa kwa kiasi cha US$200,000 kwa mwaka, wakati ushuru wa Serikali za Mitaa ni 0.3% ya mapato na matumizi ya mwaka na zote zinalipwa kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo mgodi upo.

## 4.3 Kodi ya Mapato Yanayotokana na Faida

Kodi ya mashirika makubwa juu ya mapato yanayotokana na madini ni 30% ya mapato ya shirika baada ya kuondoa gharama za uendeshaji ambayo ni kiwango kilichopangwa kwa mashirika makubwa yote Tanzania. Tangu Julai 2010, kuna udhibiti (ring fencing) katika sekta ya madini Tanzania, ambapo hasara iliyotokea katika mgodi mmoja haiwezi kuondolewa

[3] "Thamani ya jumla (gross value)" ina maana ya thamani ya madini katika soko pale zinapofikia hatua ya usafishaji au mauzo, au kwa upande wa matumizi ndani ya Tanzania pale zinapowasili katika sehemu ya kufikia ndani ya Tanzania.

kwa kutumia faida kutoka mgodi mwingine, hata kama migodi yote miwili inamilikiwa kisheria na mhusika huyo huyo mmoja (PricewaterhouseCoopers, 2012). Kusudi lake ni kuongeza kodi inayotakiwa kulipwa kwa kiwango kikubwa kadiri iwezekanavyo.

Kodi ya zuio kwa gawio zilizolipwa na kodi za ugawaji wa faida za matawi kwa wasio raia ni 10% ya jumla yote kiwango cha kodi ya zuio kwenye riba ya mkopo au riba iliyolipwa kwa wahusika ni 10% ya thamani ya jumla lakini haitatozwa kwa riba iliyolipwa kwa taasisi ya fedha ya hapa nchini.

Tanzania pia ina utaratibu wa kukopa na kurejesha mkopo pamoja na riba baadaye hususan kwa sekta ya petroli. Chini ya utaratibu huu mkandarasi hutoa fedha za mchango wa Serikali kwa ajili ya maendeleo ya mradi kisha huja kulipwa baadaye pamoja na riba kutokana na mapato ya baadaye ya Serikali (IMF, 2014).

# 5. MATUMIZI YA MAPATO NA USIMAMIZI KWA SEKTA YA MADINI TANZANIA

## 5.1 Taasisi muhimu zenye wajibu katika matumizi ya mapato na usimamizi

Taasisi ambazo zinahusika katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato Tanzania ni pamoja na zifuatazo:

### 5.1.1 Wizara ya Nishati na Madini

Wizara ya Nishati na Madini ina wajibu wa kuongoza maendeleo ya sekta ya madini kupitia kitengo chake cha madini. Kitengo cha madini hutoa mwongozo kuhusu fursa za uwekezaji; ruzuku ya leseni; vibali na idhini kwa masuala yanayohusu madawa ya ulipuaji miamba (baruti), biashara ya madini, uwekaji wa vifaa migodini, mauzo ya madini nje ya nchi na uingizaji ndani ya nchi, utafutaji na uchunguzi wa madini, uchimbaji na uchakataji madini, pia hutoa msaada / huduma kwa wachimbaji wadogo (MoEM, 2015)

Wizara ya Nishati na Madini ina wajibu wa kutoa leseni na kukusanya ada zinazoambatana nazo, ikiwa ni pamoja na ada za kodi ya mwaka na gharama nyingine. Wajibu mkubwa wa Wizara, kama ilivyo katika Sera ya Madini ya 2009, ni "kuchochea na kuongoza uwekezaji wa sekta binafsi kwa kusimamia, kutoa kanuni na kuwezesha ukuzaji wa sekta kupitia mfumo uliopangwa vizuri na wenye ufanisi". Chini ya Sera ya Uchimbaji Madini, wajibu wa Wizara ni utayarishaji kanuni, ukuzaji na utangazaji, uwezeshaji na utoaji wa huduma.

### 5.1.2 Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA)

Sera ya Madini 2009 ilitoa tamko kuhusu hitaji la taasisi ya ukaguzi ambayo itafanya kazi hiyo kwa madini ya aina zote kwa migodi mikubwa, ya kati na midogo. Sera ilikuwa inachukua hatua kutokana na upungufu ambao ulibainishwa katika utawala wa sekta ya madini. Upungufu huo ni pamoja na watumishi kuwa na ujuzi usiotosheleza, ufinyu wa maeneo ya kazi zilizoainishwa vizuri (kazi zilizoainishwa zilihusu madini ya dhahabu peke yake), ufinyu wa fedha, kukosa uhuru wa uamuzi na kiwango dhaifu cha mahusiano na uratibu na sekta nyingine. Novemba, 2009, Serikali ilianzisha Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA), taasisi huru kwa kiasi fulani, iliyopewa jukumu la kufanya ukaguzi wa fedha na mazingira pamoja na ukaguzi wa ubora na kiasi cha madini kilichozalishwa na kupelekwa nje ya nchi kwa mauzo na wachimbaji ili kuongeza manufaa kwa Serikali kutoka sekta ya madini kadiri inavyowezekana kwa maendeleo endelevu ya nchi (TMAA, 2014). TMAA ilianzishwa kwa Notisi ya Serikali No. 362 chini ya Sheria ya Mashirika Tendaji Kif. 245. Ilichukua kazi ambazo kabla ya hapo zilikuwa zikifanywa na Seksheni ya Madini na Ukaguzi chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

TMAA hutembelea migodi mikubwa kila mwaka. Hukagua taarifa/nyaraka zilizoandikwa na kuhifadhiwa, ikiwa ni pamoja na muhtasari wa taarifa muhimu za uhasibu na viambatanisho vingine na hati za madai. Baada ya kutembelea, huandika taarifa yenye hitimisho zao kuhusu mirabaha na kodi mbalimbali (ikiwa ni pamoja na kodi ya mapato) msisitizo ukiwa katika kulinganisha dhima / deni la kodi na malipo halisi. Taarifa ya mwisho ya ukaguzi iliyoandaliwa na TMAA huwasilishwa kwa Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Fedha na Mipango ya Uchumi, na Kamishna Generali wa TRA na

### 5.1.3 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Mamlaka ya Mapato Tanzania ni mhusika muhimu katika usimamizi wa mapato kwenye sekta ya madini. Inasimamia kodi zote zinazohusu sekta. Hii ni pamoja na kodi za mapato (inajumuisha kodi ya mapato ya mashirika makubwa, kodi za ajira, na kodi za zuio) na kodi ya ulaji, hasa VAT na ushuru wa forodha. Kodi katika sekta ya madini zinashughulikiwa na Idara ya Walipaji wa Kodi Kubwa, TRA. TRA ilianzishwa kwa sheria Namba 11 ya Bunge ya mwaka 1995, na ilianza shughuli zake tarehe 1 Julai 1996.

## 5.2 Mipango inayotawala usimamizi wa mapato Tanzania

### 5.2.1 Mikataba ya Maendeleo ya Kuendeleza Madini (MDAs)

Sheria ya Uchimbaji Madini ya 1998 ilimruhusu Waziri wa Madini kuingia katika mikataba ya kuendeleza madini na makampuni ya uziduaji. Hii mikataba ilijumuisha ibara zilizokuwa zinadhibiti masharti ya fedha ambayo ilibidi wajadiliane na makampuni ya uchimbaji madini. Kama sehemu ya mabadiliko (reforms), Kamati ya Serikali ya kujadili (mikataba) ilianzishwa mwaka 2007 kupitia mikataba ya kuendeleza madini na uziduaji iliyokuwepo kwa lengo la kuhakikisha pande zote mbili zinanufaika. Hivi sasa, chini ya sheria ya uchimbaji madini ya mwaka, 2010, ili kuhakikisha haki za pande zote mbili zinaainishwa vizuri na zinalindwa, wamiliki wa Leseni Maalum za Uchimbaji Madini (kwa uwekezaji unaozidi US$100 milioni) wanaweza kuingia katika MDA na Serikali. Mfano mmoja wa MDA ulitiwa sahihi Octoba 2015 kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya Magnis Resources Limited kwa makubaliano kuhusu mradi wa "Nachu Graphite Project" nchini Tanzania. Masharti muhimu waliyokubaliana yameorodheshwa kwa kifupi kama ifuatavyo:

i. Umiliki wa bure wa 5% ya hisa zote katika mradi kwa Serikali ya Tanzania;
ii. Uwezekano wa Serikali kununua 10% zaidi ya mradi kwa "thamani ya haki ya soko" kama itakavyoainishwa kwa thamani inayotambulika kimataifa;
iii. Udhibiti wa fedha utakaohakikisha kuwa kodi zote, mirabaha, na ushuru zinadumu hivyo hivyo (hazibadiliki) kwa muda wote wa MDA na
iv. Vifungu vinavyozuia aina yeyote ya utaifishaji wa mradi[4].

Ni jambo linalohitaji mjadala kuamua kama MDAs zina manufaa kwa Serikali au hapana. Kwa mfano katika tamko kwa waandishi wa habari, Magnis Resources walisema kwamba masharti waliyopata ni mazuri kuliko ambavyo wangeweza kupata katika tawala nyingine za jinsi hiyo. Kwa hiyo, wakati hali hii ni nzuri kwa kuvutia uwekezaji, lakini pia, ilipunguza mapato ambayo Serikali ilipaswa iyapate. Kwa nyongeza, MDA una vifungu ambavyo vinatamka kuwa makubaliano hayo yanaweza kupitiwa upya tena baada ya miaka 10, jambo ambalo linaweza kumaanisha kwamba mapitio yoyote mapya ya kifedha hayawezi kufanyika kwa shirika lenye MDA na Serikali.

**5.2.2 Uwazi katika Matumizi ya Mapato ya Sekta ya Uchimbaji Madini**
Tanzania ilijiunga na Mpango wa Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji Ulimwenguni mwezi Februari 2009 kufuatia sehemu ya mapendekezo ya mwaka 2007 yaliyotokana na Utafiti wa Mapitio ya Sekta ya Madini. Nchi ilianzisha Mpango wa Uwazi Katika Tasnia ya Uziduaji Tanzania (TEITI) kufanyia kazi masuala yote yanayohusu uwazi katika tasnia, ya uziduaji, sambamba na masharti ya EITI. TEITI ni mpango ulio na wadau mbalimbali wenye madhumuni ya kuongeza uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji Tanzania (TEITI, 2015).

Septemba 2015, Tanzania ilionekana kutokidhi masharti ya EITI kutokana na uchelewaji katika uchapishaji wa taarifa ya nne (2012/2013) kama inavyotakiwa kwa vigezo vya EITI. Tunaelewa kuwa huu uchelewaji katika utoaji wa taarifa unatokana hasa na uchelewaji katika kupata huduma ya msimamizi huru. Tanzania inafanya juhudi kiasi fulani katika kukidhi matakwa ya EITI, lakini uchelewaji fulani katika utoaji wa taarifa za kulinganisha na nyingine (reconciliation) kwa muda unaotakiwa kama inavyotakiwa katika masharti ya EITI unaonyesha kuwa bado kuna changamoto na uthabiti wa udhibiti ili kuhakikisha kanuni zinafuatwa (TEITI, 2014; TEITI, 2015).

**5.2.3 Mikataba ya Uwekezaji wa Nchi Mbili (BITs) na Mikataba ya Tozo la kodi maradufu (DTTs)**
Serikali ya Tanzania imepiga hatua katika kuvutia uwekezaji kwa kutoa motisha za kifedha zilizo na uwiano mzuri na zenye ushindani kwa wawekezaji. Hii kwa ni wawekezaji wa kimatiafa na wa ndani, kwa lengo la kuvutia uwekezaji mpya. Kwa nyongeza Serikali ilitia sahihi mikataba mipya ya uwekezaji wa nchi mbili (BITs) ambayo inalenga kuvutia na kulinda uwekezaji mpya na uliopo. Pia ilitia sahihi mikataba ya tozo la kodi maradufu (DTTs) na nchi mbali mbali.

Hadi hivi sasa, Serikali ya Tanzania imewekeana sahihi (BITs) na Serikali za Ujerumani, Italia, Finland, Korea ya Kusini, Netherlands, Uingereza, Sweden, Denmark, Canada, Switzerland, Thailand, China, Oman, Kuwait na Zimbabwe. Kwa upande mwingine, Serikali ya Tanzania, imeingia katika DTTs na Serikali za Uingereza, Italia, Sweden, Norway, Denmark, Finland, Korea ya kusini, Switzerland, Oman, Malaysia, Thailand, Canada, Netherlands, na Kuwait. Tanzania pia ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Dhamana ya Uwekezaji (MIGA), Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID) na imeweka sahihi Sheria ya Biashara ya Kimataifa ya Kamati ya Umoja wa Kimataifa (UNCITRAL) (BOT et al., 2013).

**5.2.4 Manufaa ya Jamii Kutokana na Uchimbaji Madini**
Kutokana na kwamba jamii zilizo karibu na migodi huathirika na shughuli za uchimbaji, baadhi ya nchi hujaribu kuhakikisha kuwa sehemu ya mapato ya sekta ya madini inatengwa ili kuzirejesha kwenye maeneo ya migodi na jamii ambako miradi ya uchimbaji madini inaendeshwa. Lakini, nchini Tanzania, mapato yanayokusanywa kutokana na shughuli za uchimbaji madini yanatakiwa yapelekwe kwenye Serikali Kuu ambako yatapangwa upya kama sehemu ya rasilimali kuu kwa kuwa mapato yanayotokana na kodi ni sehemu ya mfuko wa jumla wa hazina ya Serikali. Hii ina maana kwamba mapato yanayotokana na madini yanaweza kurejeshwa kwa jamii zinazoishi kwenye maeneo ya uchimbaji madini kwa kupitia utengaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya jumla ambayo yamepitishwa katika mchakato wa bajeti ya Serikali (ICMM, 2009). Wakati hii inaweza kuchukuliwa kama kutokuwa makini na mahitaji ya jamii za migodini, inawezekana kuwa na sababu za kuridhisha kwa utaratibu huu nchini Tanzania. Mapato yaliyo mengi yanayotokana na madini yanatoka katika wilaya sita tu kati ya jumla ya wilaya 117 na kuna wilaya nyingi ambazo ni maskini zaidi kuliko hizo ambazo ziko sehemu zenye migodi ambapo uchimbaji madini hufanyika. Kwa hiyo, wilaya ambapo uchimbaji hufanyika hutegemewa kufurahia ngazi ya juu zaidi ya mapato kuliko wilaya hizi ambazo ni maskini zaidi, kwa hiyo kutumia mapato kutoka wilaya zenye uchimbaji wa madini kwa ajili ya hizo ambazo ni maskini zaidi kunaweza kusiwe na ubaya wowote. (ICMM, 2009).

[4] Maelezo zaidi yanapatikana katika tamko la Magnis Resources Limited kwa waandishi wa habari kutangaza MDA katika tovuti: http://magnis.com.au/article.php?id=120 iliyopatikana tarehe 12 Desemba 2015.

Lakini, taarifa ya Oxford Policy Management, iliyopewa kazi na Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2011, inaonyesha kuwa manufaa ya kuishi katika maeneo ya uchimbaji yanaweza kuwa hayaonekani, hali inayoonyesha hitaji la aina fulani ya fidia kutoka kwa Serikali. Taarifa hiyo, ambayo inatokana na utafiti uliofanywa kuhusu migodi minne (Mgodi wa Dhahabu wa Geita, Mgodi wa Almasi wa Mwadui na Migodi ya Dhahabu ya Bulyanhulu na wa Buzwagi) ilionyesha kwamba wahojiwa wengi wana maoni hasi kuhusu manufaa ya uchimbaji madini. Jamii kwa ujumla haioni kuwa migodi imetoa fursa nzuri za ajira na manufaa. Uwepo wa uchimbaji mkubwa umeongeza pengo la usawa kati ya wale wanaopata manufaa kutokana na migodi na wale wasiopata na kusababisha mifarakano katika baadhi ya jamii. Watu wenye ajira migodini wanakuwa na mapato kuliko wale ambao hawana, hali inayoleta manung'uniko kuhusu uwepo wa "ngazi mpya" ya watu (Oxford Policy Management, 2011). Hao waliobaki bado wanahitaji watazamwe kwa namna fulani na Serikali.

Makampuni ya uchimbaji madini yamekuwa pia yakiwekeza baadhi ya faida zao katika Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR) ili kuongeza uwepo wao, kukubalika, na kujenga mahusiano na jamii. Baadhi ya juhudi hizi zimeonekana katika maeneo ya elimu, afya, maji na barabara. Acacia (zamani African Barrick Gold) iliandaa mfuko wa maendeleo ya jamii, uliojulikana kama "Maendeleo Fund", mwaka 2011 kama sehemu ya mkakati wake wa CSR na tangu wakati huo imetumia zaidi ya US$ milioni18 kwa ajili ya kufadhili miradi ya elimu, afya, usafi wa mazingira, maji, miundombinu, kuboresha maisha, na mingine (Concern for Development Initiatives in Africa (ForDIA), 2012). Jumla ya US$ milioni 11.5 pia zilitumiwa na Kampuni ya African Barrick Gold kwenye miradi ya maendeleo ya jamii mwaka 2013; kati ya hizo US$ milioni 5.4 zilitumika kwa ajili ya elimu na afya (African Barrick Gold, 2014). Mwaka 2010, African Barrick ilitoa ruzuku ya shilingi milioni 50 za Tanzania kwa ajili ya waathirika wa mafuriko katika Wilaya ya Bukombe; pia ilianzisha mfuko wa maafa na kutumia shilingi milioni 22.6 kuwapeleka mafunzo wajasiriamali 30 kutoka kijiji cha Kakola, kata ya Bugarama, Wilaya ya Kahama (Poncian, 2015).

Ingawa miradi ya CSR inaweza kuonekana kama imetokana na wawekezaji wenyewe, Serikali pia inapaswa kupongezwa, kwani Sera ya Madini ina kipengele kinachosisitiza 'ujengaji wa uhusiano baina ya makampuni ya uchimbaji madini na jamii zinazozunguka migodi', ambapo kampuni za uchimbaji madini zinahimizwa kuchangia maendeleo ya jamii kupitia sera zao za CSR. Aidha, ieleweke kwamba ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa sehemu ya mapato yanayotokana na sekta ya madini yananufaisha jamii badala ya kunufaisha makampuni ya madini peke yake. Kwa hiyo, CSR inatakiwa ionekane kama ni wajibu wa hiari wa makampuni ya madini badala ya kuonekana kama ni lengo la sera ya Serikali. Katika nchi nyingine, serikali kwa kawaida hupoteza mapato mengi ya kodi, kwa kuwa makampuni hutumia CSR kukwepa kodi. Lakini hali haionekani kuwa hivyo Tanzania, kwani haijaruhusiwa kutoa CSR kutoka kwenye kodi ya mapato. Serikali inahitaji kujitahidi kutimiza wajibu ambao kampuni zinafanya kupitia CSR, kwa kuwa AMV inatarajia zaidi kutoka kwa Serikali ili jamii zinazozunguka migodi zinufaike.

**5.2.5 Mfuko Maalum wa Mapato**

Tanzania pia iko katika hatua ya mbele katika kuanzisha mfuko maalumu wa matumizi ya mapato maalum, msisitizo ukiwa katika gesi asilia. Sera ya Gesi Asilia ya 2013 inashauri Mfuko wa Mapato ya Gesi Asilia uanzishwe na kusimamiwa kuhakikisha uwazi na uwajibikaji kuhusu ukusanyaji, ugawaji, matumizi, na usimamizi wa mapato yote yanayotokana na gesi asilia (ESRF, 2014). Matokeo yake, Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi Asilia, iliwekwa mwaka 2015 mwezi Julai ili kutekeleza hiyo sera. Chini ya Kifungu cha 8 cha sheria hiyo, malengo ya mfuko huo ni kuhakikisha kwamba:

i. Uthabiti wa fedha na uchumi mkubwa ni endelevu;
ii. Upatikanaji wa fedha za kuwekeza katika mafuta na gesi ni wa uhakika (umedhaminiwa);
iii. Maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi yanaongezeka na
iv. Rasilimali kwa ajili ya vizazi vijavyo zinalindwa.

Vyanzo vya fedha za mfuko huu vimeainishwa katika Kifungu cha 9 cha sheria hiyo kama:

i. Mirabaha;
ii. Mgawo (hisa) wa faida za Serikali;
iii. Gawio la Serikali kutokana na kushiriki kwake katika shughuli za mafuta na gesi;
iv. Kodi ya mapato ya shirika kutokana na uchunguzi, uzalishaji na maendeleo ya rasilimali ya mafuta na gesi na
v. Marejesho kutokana na uwekezaji wa mfuko.

Kuhakikisha kuwa mfuko hautumiki vibaya, Kifungu cha 11 cha sheria kinatoa vizuizi kuhusu matumizi ya mfuko. Fedha zilizohifadhiwa katika mfuko hazitatumika kwa: (a) utoaji mikopo kwa Serikali, mashirika ya umma ya biashara, sekta binafsi (watu mashirika / chombo chochote au mtu mwingine yeyote au chombo kingine; (b) kama dhamana au rahani au masharti/ ahadi au madeni ya mtu / chombo kamili kisheria (c) Kwa kuhonga au kwa vitendo vingine vya rushwa, ubadhirifu au uwizi.

Ingawa Tanzania ina mfuko maalumu wa matumizi ya mapato kwa gesi asilia pekee, imechukua hatua muhimu kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo wanapatiwa sehemu yao. Aidha, ni muhimu kwamba mifuko kama hii ianzishwe kwa rasilimali nyingine za madini.

# 6. MWONGOZO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI KUHUSU SEKTA YA UCHIMBAJI MADINI

Msingi wa mikakati ya sekta ya madini katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Ibara ya 114 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayosisitiza usimamizi wa maliasili. Chini ya Ibara ambayo inayosisitiza usimamizi wa sekta ya mali asili, nchi wanachama zinakubaliana, pamoja na mambo mengine, kuzingatia uandaaji wa mazingira wezeshi kwa uwekezaji katika sekta ya madini na kuoanisha kanuni za uchimbaji madini ili kuhakikisha taratibu ambazo ni rafiki kwa mazingira na uchimbaji madini zinafuatwa.

Hati ya Awali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Mazingira na Rasilimali za Mali Asili inaweza kuchukuliwa kama utaratibu wa utawala wa kisera ambao umefanyika katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu sekta ya uchimbaji madini. Hata hivyo, hati ya awali yenyewe bado haijaanza kutumika, kwa kuwa Tanzania bado haijaipitisha. Ibara ya 18 ya hati hiyo ya awali inazungumzia sekta ya uchimbaji madini, miongoni mwa masuala mengine inasema kuwa nchi wanachama zitaandaa na kuratibisha sera ya pamoja, sheria, na mikakati ya kufikia na kuchimba / vuna rasilimali ya madini kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii kwa ujumla. Nchi wanachama pia ziliazimia kuandaa mikakati kuhusu uzalishaji endelevu, uongezaji thamani, na masoko ya madini na bidhaa zake, taratibu za ufanisi zikiwa zimewekwa ili kudhibiti biashara ya rasilimali asilia katika jamii. Shughuli zote zilizokuwa zimepangwa zimesitishwa kwa sasa, kwa kuwa Tanzania bado inashauriana na wadau kabla ya kuipitisha hiyo hati ya awali.

Majadiliano wakati wa Mkutano wa 5 wa kipindi cha kwanza cha Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki uliofanyikia Kigali, Rwanda tarehe 12 – 26 Aprili 2013 pia yanaonyesha kuwa kuna juhudi fulani zinazofanyika katika ngazi ya sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuandaa mikakati ambayo ni hatua kubwa katika kufikia ajenda za AMV.

Mpango wa kuwezesha maendeleo ya uziduaji na uchakataji wa madini sasa hivi unaandaliwa kwa msaada wa kitaalamu wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. Malengo ya mradi huu yanajumuisha:

(a) Mapitio ya kanuni, sera na sheria zinazotawala tasnia ya uziduaji na utengenezaji / usafishaji madini kwa malengo ya kufanya hizo kanuni kuwa za msaada zaidi katika maendeleo ya tasnia ya uziduaji na kuongeza thamani ya madini;
(b) Kuimarisha uwezo wa kikanda na kitaifa katika sera ya maendeleo ya madini na
(c) Utambuzi wa fursa za uwekezaji katika tasnia ya uziduaji na uongezaji wa thamani ya madini.

Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya tathmini ya maliasili zilizoko katika kanda zenye uwezo wa kuongezewa thamani mumo humo ndani ya kanda ili kutengeneza ajira na kuhakikisha jamii zinapata manufaa makubwa kadiri inavyowezekana kutokana na rasilimali za madini zilizopo katika kanda. Juhudi zinazoelekezwa katika kulinganisha / kusawazisha sera za madini na utawala wake katika nchi wanachama ilisemekana kuwa zimeanza. Maeneo yanayosisitizwa katika kuoanisha yanajumuisha: ufikiaji na umiliki wa ardhi; ufikiaji na umiliki wa madini; mirabaha ya madini kwa Serikali; taratibu za kufuata kwa ajili ya Tathmini ya Matokeo katika Mazingira na Ufuatiliaji wa Mipango ya mazingira; utawala wa kodi; manufaa kwa jamii wakati na baada ya uchimbaji; uongezaji wa thamani kwa madini na ajira pia maendeleo ya ujasiriamali zinazofuatia; wajibu wa jamii, mamlaka za kijamii, Serikali Kuu, na kampuni za uchimbaji madini; utafutaji masoko kwa madini; utengenezaji ajira na maendeleo ya rasilimali watu (Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2013).

Kwa kutokuwepo hati ya awali kuhusu uchimbaji madini, hapakuwa na kitu chochote ambacho sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ingetumia kuhakikisha kwamba utawala wa fedha za sekta ya uchimbaji madini kwa nchi wanachama pamoja na jinsi wanavyotumia rasilimali zinazotokana na sekta ya hiyo zinaenda sawasawa na vifungu vya AMV. Kwa hiyo, wakati tayari kuna majadiliano yanayoendelea na yenye mwelekeo mzuri, utekelezaji wa AMV bado uko mbali, kutokana na ukosefu wa uelewa wa pamoja wa mchakato wa uchimbaji madini, kama inavyoonyeshwa na kukataa kwa Tanzania kuweka sahihi au kupitisha Hati ya Awali ya Usimamizi wa Mazingira na MaliAsili.

# 7. TATHMINI: KUOANISHA NA KUPANGA KWA KINA AMV KATIKA NGAZI YA TAIFA

Shughuli zinazofanyika katika ngazi ya nchi kwa ujumla zinaonyesha kuwa Tanzania iko katika mchakato wa kuhakikisha inatimiza vifungu vya AMV kuhusu sekta ya uchimbaji madini. Hivi sasa, nchi iko katika hatua za kuandaa Dira ya Taifa kwa msaada wa AMDC, ambapo hatua fulani zimekwishachukuliwa. Wakati kuna mafanikio kidogo sana katika mabadiliko ya yenyewe hasa ya kugeuza utawala wa fedha katika sekta ya madini kama inavyotakiwa katika AMV, inatia moyo kwamba hii kazi imeanza na inaendelea. Sehemu hii inatathmini utawala wa fedha katika sekta ya madini Tanzania kwa kulinganisha na kile kinachotakiwa katika AMV na kupima pengo lililopo kufuatana na malengo ya AMV. Kwa hiyo, hii tathmini ya kuoanisha na kupanga AMV itaangalia tu udhibiti wa fedha katika sekta ya madini pamoja na usimamizi wa matumizi na mapato.

## 7.1 Kuoanisha na Kupanga kwa Kina Utawala wa Fedha katika Sekta ya Uchimbaji Madini Tanzania

Mojawapo ya malengo ya AMV ni kuhakikisha kuwa utawala wa sekta ya madini unatoa thamani au unaleta manufaa kwa nchi baada ya kipindi fulani. Hii ni pamoja na kuboresha usimamizi wa malipo ya uhawilishaji yanayohusu shughuli za uchimbaji madini. Chini ya Mpango wa Utekelezaji wa AMV, juhudi za kufanikisha hili kwa kawaida zinaonekana zaidi katika mikakati inayoelekezwa katika kuhakikisha kuwa kuna ongezeko la mgawo wa mapato ya madini kwa nchi za Afrika zinazoshughulika na uchimbaji madini. Kuangalia viashiria vya ufuatiliaji vilivyobainishwa kutasaidia kuonyesha hali ilivyo Tanzania kuhusu ufikiaji wa malengo ya AMV:

**a. Kuboresha uwezo wa taifa wa kukagua uzalishaji wa madini na mauzo nje ya nchi**

Sera ya Madini ya 2009 ilishuhudia uhamishaji wa kazi ambazo hapo nyuma zilikuwa zikitekelezwa na Kitengo cha Ukaguzi wa Madini kwa shirika huru la "Shirika la Ukaguzi wa Madini Tanzania", (TMAA). Kiashiria cha ufuatiliaji ili kuhakikisha vifungu vya AMV vinatekelezwa kama vilivyo katika Mpango wake wa Utekelezaji ni "uwepo wa mfumo wa ukaguzi na unaotekelezwa kwa kutumia mainspekta waliofunzwa". Mtazamo katika shughuli za TMAA, kama zilivyotolewa taarifa katika taarifa zake za mwaka, ambazo zinaonekana kwa uwazi na umma katika tovuti yake, zinaonyesha kuwa sasa inao wataalamu katika tasnia hii na imechangia vizuri katika ongezeko la mapato yanayotokana na sekta ya madini. Kwa mfano, ukaguzi wa taarifa / nyaraka za fedha na mapitio ya kodi yaliyofanywa na TMAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) umesaidia kuharakisha malipo ya kodi ya kampuni ya Geita Gold Mine Limited (GGML) inayomilikiwa na AngloGold Ashanti Limited. Ukaguzi wa taarifa / nyaraka za fedha na mapitio ya kodi yaliyofanywa na TMAA mwaka 2014 zilipelekea ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambayo yalikuwa hayajalipwa kama ifuatavyo:

i. Kodi ya zuio ya kiasi cha TZS milioni 905.5 ambazo hazikulipwa kutoka katika malipo yaliyofanywa kwa ajili ya watoaji huduma za kiteknolojia katika uchimbaji madini;
ii. Mirabaha ya kiasi cha TZS milioni 761.3 na mfuko wa kujenga uwezo/nguvu wa kiasi cha TZS milioni 336.7;
iii. Ushuru wa Maendeleo ya Stadi (SDL) kiasi cha TZS milioni 150.9;
iv. Ushuru wa Huduma kiasi cha TZS bilioni 2.77.

Ukaguzi wa fedha wa mara kwa mara uliofanywa na TMAA umeboresha utunzaji wa nyaraka za fedha na umefanya makampuni makubwa ya uchimbaji madini kufuata kanuni zilizowekwa (TMAA, 2014).

Mfumo wa utawala wa ukaguzi katika sekta ya madini Tanzania umeboresha kwa kiwango kikubwa uwezo wa nchi kukagua uzalishaji madini na mauzo ya nje kivitendo, kama inavyotakiwa katika matarajio ya AMV.

**b. Kufanya mapitio ya udhibiti wa madini kwa lengo la kuongeza mapato**

Kwa kutegemea viashiria vya ufuatiliaji kama vilivyotolewa kwenye Mpango wa Utekelezaji wa AMV, mafanikio ya kiashiria hiki yatapimwa kwa 'mapitio ya mfumo wa utawala wa madini na kiwango cha kuboreshwa kwa mapato ya fedha zilizokusanywa na nchi za Kiafrika zinazoshughulika na uchimbaji madini'. Tanzania ilifanya mabadiliko mengi katika mfumo wa kodi, hasa baada ya uwekwaji wa Sera ya Madini ya 2009. Sababu mojawapo ya mabadiliko haya ilikuwa kuongeza mapato kutokana na sekta, ambayo yalifanya mirabaha pia kuongezeka. Haya mapitio pia yalihusisha gharama za leseni ambapo mfumo mpya wa utawala wa utoaji leseni ulianzishwa. Kwa hiyo mapitio kweli yalifanyika kwa lengo la kufikia kiwango cha juu kadiri iwezekanavyo cha mapato. Kinachopasa, lakini, ni kuhakikisha ni kwa kiwango gani mapitio yalifanikisha ufikiaji wa kiwango cha juu kabisa cha mapato kutokana na sekta ya uchimbaji madini.

Mapato ya kodi ya sekta ya uchimbaji madini kutoka katika migodi mikubwa kama asilimia ya jumla ya mapato yote ya kodi yaliongezeka toka 2.41% mwaka 2001 hadi 4.41% mwaka 2014. Mwaka 2009 mabadiliko ya kodi yalipoanzishwa kupitia sera ya uchimbaji madini, mapato ya kodi kutoka migodi mikubwa yalikuwa karibu 3.10%. Hii imeongezeka hadi 4.41% mwaka 2014, ijapokuwa bei za bidhaa katika masoko ya kimataifa imepungua, jambo ambalo limeathiri pia mapato yanayotokana na uchimbaji madini. Hii inaonyesha pia kuwa mabadiliko kwa ujumla yameleta ongezeko katika mapato ya sekta ya madini. Hata hivyo, haiko wazi iwapo ongezeko hili limefikia kiwango cha juu kadiri inavyowezekana. Hii ni kweli kwani mapato yanayotokana na sekta ya uchimbaji madini kama asilimia ya jumla ya mapato ya kodi zote yalifikia kiwango cha juu mwaka 2012 hadi karibu 10.97%, baada ya kufikia kiwango kikubwa pia cha 5.75% mwaka 2011. Kwa hiyo kama hivi viwango viwili vya juu vinaakisi uwezo uliofichika wa sekta ya uchimbaji madini, mfumo wa utawala wa mapato bado haujafikia kiwango cha juu kabisa kinachowezekana kufikiwa.

Kwa hiyo, wakati kuna ishara kwamba uwezo wa upatikanaji wa mapato yanayotokana na kodi ya sekta ya madini Tanzania umeongezeka, kuna ishara kwamba kiasi kinachokusanywa kwa sasa hakijafikia kiwango cha juu kwa kadiri inavyowezekana.

**c. Kujenga uwezo na kuimarisha stadi za maofisa kujadili masuala ya fedha na kufuatilia kwa ufanisi kuhakikisha uzingatiaji wa sheria za kodi**

Chini ya Mpango wa Utekelezaji wa AMV, kiashiria cha ufuatiliaji cha kuhakiki ufuataji wa sheria/kanuni ni ongezeko katika idadi ya watunga sera na wadau wengine wanaoshiriki katika mipango ya kujenga uwezo. Ni muhimu kujua kuwa sehemu ya huu wajibu hutekelezwa na TMAA, ambayo tayari ina ujuzi katika ukaguzi, kutokana na kujengewa uwezo na taasisi mbalimbali. Lakini, ni muhimu pia kwa maofisa wa Serikali walioko katika ngazi ya utungaji sera kushiriki katika mipango hii ya ujenzi wa uwezo ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi. Washirika wa maendeleo kwa kawaida wamekuwa wakiwezesha mipango hii ya kujenga uwezo kwa maofisa wa Serikali.

Tanzania tayari iko katika mchakato wa kuhakikisha ufuataji wa vifungu vya AMV. Kwa mfano, mwaka 2014, Ofisi ya UNDP nchini Tanzania ilipokea maombi rasmi kutoka Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa ajili ya msaada katika kutengeneza Dira ya Uchimbaji Madini Tanzania, sambamba na vifungu vya AMV. Ombi hili liliwafanya UNDP na AMDC wawezeshaji wa CMV, Wizara ya Nishati na Madini ikiwa taasisi ya kiserikali inayoongoza jopo hilo. Shughuli mahsusi za ujengaji uwezo chini ya AMDC kwa ajili ya kuhakikisha ufuataji wa masharti AMV zilifanyika, jambo ambalo ni la maendeleo chanya.

Mwaka 2012 Wizara ya Nishati na Madini ya Serikali ya Tanzania iliomba Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Kiswidish (Sida) msaada wa kuimarisha uwezo wa Wizara hiyo kusimamia sekta ya madini. Hili ombi likawaleta pamoja Kikundi cha Maendeleo ya Mikakati Endelevu (Sustainable Development Strategies Group (SDSG) na Taasisi ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu (International Institute for Sustainable Development (IISD), kwa kushirikiana na Kituo cha Mafunzo ya Sera ya Biashara Afrika (Trade Policy Training Centre in Africa (TRAPCA) na Benki ya Dunia (World Bank), wakaendesha mafunzo / semina ya siku tano kuhusu majadiliano ya mikataba ya maendeleo ya migodi. Warsha, hiyo iliyoandaliwa kwa ajili ya maofisa wa Serikali wa ngazi ya juu wanaoshughulika na majadiliano ya kimikataba, ilifanyika toka Mei 26 hadi Mei 30, 2014 Arusha, Tanzania. Semina ilikuwa na lengo la kuongeza ujuzi na stadi za wawakilishi wa serikali Barani Afrika juu ya majadiliano ya mikataba ya maendeleo ya migodi na wawekezaji wa nje[5].

Kwa hiyo kwa ujumla, kuna uthibitisho kwamba Serikali ya Tanzania imechukua hatua mahsusi katika kuimarisha uwezo na stadi za maofisa wanaohusika na sekta ya uchimbaji madini kwa lengo la kujadili masuala ya kifedha. Hata hivyo waandishi hawakuweza kufahamu idadi halisi ya watumishi waliopata mafunzo, ambayo ingehitajika ili kutathmini kama hiyo idadi imekuwa ikiongezeka kama kiashiria cha AMV kinavyotaka.

**d. Kurejea au kurejea tena mikataba kwa lengo la kuongeza mapato na kuhakikisha nafasi ya fedha na usimamizi wa mapato yasiyotegemewa**

Mabadiliko katika usimamizi wa sekta ya uchimbaji madini Tanzania, ili kuongeza mapato pia yalileta mabadiliko katika mikataba ya makampuni ya uchimbaji madini iliyokuwepo. Tanzania imezifanya leseni za uchimbaji madini kuweza kupatikana kwa upya (renewable) na kwa kila ombi jipya, masharti mapya yanajadiliwa tena kutegemeana na sera ya uchimbaji madini kwa wakati husika. Tanzania hupoteza uhuru wa kurejea upya masharti ya fedha kupitia mikataba ya kuendeleza madini na uziduaji (MDAs) wakati ambapo majadiliano mapya yanaweza kufanyika tu baada ya kipindi fulani. Wakati katika mwongozo kwa wawekezaji ulioandaliwa na Wizara ya Nishati na Madini, maombi mapya yanapokelewa baada ya kila miaka mitano, MDA iliyojadiliwa huko nyuma, inaonyesha kuwa masharti yote yanaweza kupitiwa na kujadiliwa tena baada ya miaka 10. Hii ina maana kwamba wakati mwingine, wawekezaji wanao uwezo wa kuhakikisha kuwa masharti ya MDA yanakuwa na faida kwao kwa kuwa miaka kumi ni muda mrefu sana na kwa hakika nchi inapoteza uhuru wa kujadili kwa upya kuendana na mabadiliko mapya ya kisera.

[5] https://www.iisd.org/pdf/2014/tanzania_negotiation_seminar_announcement.pdf.

e. **Kuandaa mifumo ya kutathmini sehemu ya udhibiti wa kodi ili kuzuia uvujaji, upotevu na uepukaji kodi (mfano: uhawilishaji bei )**

Mamlaka ya Mapato Tanzania imejaribu kuwa na utawala wenye ufanisi kwa kadiri uhawilishaji wa bei unavyohusika kwa kuandaa mwongozo wa uhawilishaji bei. Malengo ya mwongozo huu ni kuwaongoza walipakodi kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika kubaini bei ambayo ni ya haki na haitokani na shinikizo toka upande wowote na kuleta taratibu linganifu katika utekelezaji wa sheria ya kodi, na kanuni zake kwa kuzingatia mazingira ya biashara Tanzania. Kwa nyongeza, kanuni za kodi ya mapato (uhawilishaji bei) za mwaka 2014 zilitungwa kama jaribio la kuzuia uvujaji haramu wa fedha kupitia uhawilishaji wa bei.

TMAA pia ina jukumu katika kuzuia usafirishaji haramu wa madini na uepukaji wa ulipaji mrabaha kwa ajili ya madini kwa kuwaweka wakaguzi katika viwanja vikuu vitatu vya ndege nchini yaani Kiwanja cha Kimataifa cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA), Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) na Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (MWZ)) ili kukagua na kubaini usafirishaji nje wa madini. Hili linafanyika kwa ushirikiano na vyombo vingine vya Serikali hasa Idara ya Madini, Mamlaka ya Ndege Tanzania, Kikosi cha Polisi Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Idara ya Uhamiaji. Dira ya Uchimbaji Madini ya Afrika (AMV) umetumia kiashiria cha ufuatiliaji kama kiwango ambacho uvujaji wa kodi umepunguzwa kwa mifumo ya tathmini kama inavyoamuliwa na kaguzi huru za ufuataji wa kanuni za kodi. TMAA imeweza kubaini na kuzuia mitiririko haramu ya fedha isitokee, jambo linaloonyesha ufanisi wake. Kwa mfano, kipindi cha mwaka 2014, madini yenye thamani ya TZS milioni 832 (sawa na US$479,263) yalikamatwa katika majaribio 27 ya usafirishaji haramu wa madini katika viwanja vya JNIA, KIA na MA. Taarifa za matukio haya zilipelekwa kwa vyombo vingine vya Serikali kwa hatua za kisheria. Tangu Julai 2012 hadi Desemba 2014, madini yenye thamani ya TZS bilioni 15.92 (sawasawa na US$9,216,590) yalikamatwa katika majaribio sitini na sita (66) tofauti ya magendo ya madini mbalimbali katika viwanja vitatu vya ndege (TMAA, 2014). Kwa hiyo, mifumo ya kuzuia uvujaji kupitia mitiririko haramu ya fedha iko imara Tanzania.

f. **Kufanya mapitio ya masharti ya mikataba ya tozo la kodi maradufu na BITs na nchi wenyeji wa makampuni ya uchimbaji madini ikiwa ni pamoja na kanuni ya kuwa madini yalipiwe kodi katika hatua ya uziduaji**

Chini ya Mpango wa Utekelezaji wa viashiria vya AMV, idadi ya mikataba ya tozo la kodi maradufu na ya mikataba ya nchi mbili iliyowekwa sahihi na kutekelezwa kati ya nchi ya Kiafrika na mshirika wake katika uwekezaji ni kigezo cha upimaji. Jambo ambalo haliko wazi ni kama kuwa na idadi kubwa ya mikataba iliyowekwa sahihi ni vizuri au ni vibaya. Ni muhimu kuelewa kuwa mikataba ya tozo la kodi maradufu kwa kawaida matokeo yake ni nchi kupoteza haki fulani za kutoza kodi kwa wawekezaji wanaotoka katika nchi ilizowekeana sahihi nao. Hili pia linaweza kuathiri uwezo wa nchi kutoza kodi madini 'katika hatua za uziduaji', kama inavyotakiwa na AMV, kwani baadhi ya vipengele vinaweza kuingizwa kuonyesha kuwa kutoza kampuni kodi nchini Tanzania kunaweza kuwa kutoza kodi maradufu kama baadhi ya kodi zimekwisha lipwa katika nchi ilikotoka (mwenyeji). Kwa nyongeza, masuala mengine kama vile utulivu wa kiuchumi na kisiasa, gharama za rasilimali na upatikanaji wa wafanyakazi kwa kawaida huchukuliwa kama ya muhimu zaidi katika kuvutia uwekezaji kuliko BITs. Kwa hiyo, idadi kubwa ya BITs zilizowekewa sahihi zinaweza zisiwe nzuri ya kutosha kwa nchi katika muda mrefu.

Hata hivyo, BITs pia zinalinda wawekezaji kwani zinaweka taratibu za kufuatwa na Serikali katika uhusiano wake na wawekezaji. Hizi hazitakiwi zionekane kuwalinda sana wawekezaji, kiasi cha kujinyima kodi ambazo zingetakiwa zilipwe kutokana na kulindwa na BITs.

Tanzania imeweka sahihi BITs na nchi zipatazo 14, na majadiliano na nchi nyingine yanaendelea. Tanzania pia imetia sahihi mikataba ya tozo la kodi maradufu DTTs na nchi 14. Hii inaonyesha kwamba Tanzania imewania kuvutia uwekezaji.

| Nchi zilizotia sahihi BIT na Tanzania | Hali |
|---|---|
| Egypt, Finland, Germany, Italy, Jordan, Korea, Republic of Mauritius, Netherlands, Oman, South Africa, Sweden, Switzerland, Turkey, United Kingdom and Zimbabwe | Kazi zinaendelea |

*Chanzo: UNCTAD (2014).*

Pamoja na hii idadi kubwa ya mikataba ambayo imeshawekewa sahihi, kama matarajio ya AMV yanavyosema, mfumo wa kodi Tanzania bado umeundwa kwa kuhakikisha kuwa kodi inalipiwa Tanzania (kwenye chanzo), hata kama wawekezaji wa nje wanahusika. TMAA nayo imehakikisha sheria / kanuni zinafuatwa (compliance), kwa kuwa baadhi ya madeni ya kodi ambayo shirika la ukaguzi (TMAA) imebainisha kwa miaka ni madeni ambayo wadaiwa ni makampuni ya kigeni. Mirabaha nchini Tanzania inalipwa kutegemea thamani ya mauzo ya nje ya bidhaa iliyozalishwa Tanzania. Hata hivyo, bado kuna hitaji pia la kufanyia mapitio hii mikataba iliyotiwa sahihi kama AMV inavyotaka ili kuhakikisha kuwa mfumo wa utawala wa kodi haunyimi Tanzania mapato. Wakati nchi kama vile Zambia zimepitia kwa upya mikataba yao ya tozo la kodi maradufu, waandishi hawakuweza kupata mifano yeyote ya mikataba iliyojadiliwa upya tena kwa namna hiyo nchini Tanzania.

**g. Kujenga uwezo na mifumo kunadi haki ya madini pale inapofaa**

Chini ya Mpango wa Utekelezaji wa AMV, kiashiria cha ufuatiliaji kwa tarajio hili ni kiwango ambacho mifumo ya umiliki wa madini ulio na ushindani na uwazi inatekelezwa. Wakati kuna kanuni nyingi zinazotawala taratibu za mwekezaji kupata leseni, mfumo wa kupata kibali cha umiliki wa madini Tanzania hauko wazi. Vipengele vya kutilia maanani kabla ya kumpatia kibali mwekezaji, hasa panapokuwa na wawekezaji zaidi ya wawili wanaotaka vibali havijawekwa wazi kwa umma. Kuongeza uwazi kwa umma, kuna hitaji la kuunda mfumo kama huo ambao utaondoa mashaka kwa umma kwamba uamuzi uliotolewa kutoa kibali/vibali ulifanyika kwa haki, bila shinikizo au mwingiliano wowote hasi.

**h. Fursa nyingine za kuoanisha na kupanga kwa kina mfumo wa utawala wa fedha katika uchimbaji madini na AMV**

Tanzania pia imepiga hatua katika kuhakikisha kuwa madini yaliyochimbwa Tanzania yanapata thamani zaidi kupitia uongezaji thamani. Sera ya madini ya mwaka 2009 ina vifungu / vipengele vinavyohusu shughuli za uongezaji thamani kama vile: kuongeza faida ya madini, ukataji na ung'arishaji wa vito vya thamani (gemstone), utengenezaji wa shanga na mapambo, na uchongaji wa mawe. Kwa kuchukua fursa iliyotolewa na tamko la kisera, Tanzania imepata ongezeko katika: vituo vya ukataji vito, viwanda vya uchenjuaji shaba, ukataji wa miamba, na vifaa vya ung'arishaji (dimension stones) (MoEM, 2015).

Mojawapo ya maendeleo mazuri nchini ni Maonyesho ya Vito Arusha, maonyesho ya kimataifa ambayo yanafanyika Arusha kila mwaka tangu 2012. Madhumuni ya maonyesho hayo ni kuvutia ushindani katika miundombinu ya kuongeza thamani ili nchi ipate faida zaidi ya moja kwa moja kutokana na sekta ya uchimbaji madini, ikiwa ni pamoja na utengenezaji ajira. Ongezeko la thamani pia linakinga Tanzania dhidi ya kushuka kwa bei za bidhaa. Msisitizo katika viwanda vya kuongeza thamani kunaiweka Tanzania katika nafasi ya mbele katika nchi nyingi za Kiafrika, ambazo bado zinaendelea kuuza nje ya nchi bidhaa za madini ambazo ni ghafi, tofauti na matarajio ya AMV. Hatua hii imeongeza mapato katika sekta ya madini.

## 7.2 Kuoanisha na Kupanga kwa Kina Usimamizi na Matumizi ya Mapato Tanzania

Kutokana na Mpango wa Utekelezaji wa AMV, vifuatavyo ni baadhi ya viashiria muhimu vya mafanikio kuhusu uoanishaji na upangaji kwa kina wa AMV.

**a. Kuchunguza mikakati ya kuwekeza mapato yasiyotegemewa na kodi ya madini katika mfuko maalumu wa matumizi ya mapato ikiwa ni pamoja na mfuko wa udhibiti na mfuko wa miundombinu**

Tanzania iko katika hatua kubwa katika kuanzisha mfuko maalumu wa matumizi ya mapato (SWF) katika sekta ya gesi katika muundo wa Mfuko wa Mapato ya Gesi Asilia (Natural Gas Revenue Fund).Gesi asilia ni rasilimali ambayo pia inahitaji kutumiwa kwa umakini mkubwa sambamba na matarajio ya AMV. Wakati majadiliano kuhusu mfuko maalumu wa matumizi ya mapato kwa madini yaliyobaki hayajaanza vizuri bado, inategemewa kwamba uzoefu wa sekta ya gesi utatumika kama mafunzo ambayo yatasaidia katika kupanua wigo na kufikia madini mengine.

Mpango wa Utekelezaji wa AMV unatarajia idadi fulani ya SWF kuanzishwa na nchi za Kiafrika zinazoshughulika na uchimbaji madini kama lengo la muda mfupi, ambalo linaweza kukamilika katika miaka mitano. Ingawa SWF ya gesi asilia ilikuwa imeshaanzishwa tayari tangu mwaka 2016, mifuko zaidi ilikuwa inategemewa kuanzishwa chini ya AMV.

**b. Kuandaa mfumo wa usambazaji kodi kwa lengo la kugawa sehemu ya mapato yanayotokana na madini kwa jamii zinazoishi karibu na migodi pia kwa mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika.**

Kama ilivyo kwa nchi nyingi za Afrika, mfumo wa utawala wa uchimbaji madini Tanzania ni wa kwamba kodi zote ni sehemu ya mfuko wa pamoja, na unagawanywa kutegemea sera ya taifa ya fedha. Mgawanyo wa mapato hauangalii kama wilaya hii kuna mgodi au hakuna. Kwa hiyo kwa sasa, sera ya Tanzania haijaandaliwa kwa jinsi ambavyo jamii zinazoishi karibu na migodi au mamlaka zao wanapata mgawo ambao ni tofauti na migawo inayotolewa kwa maeneo ambayo hayana migodi. Hata hivyo, huu unaweza usiwe utaratibu mbaya, kwani wilaya zenye migodi nchini Tanzania siyo lazima kwamba ziwe ndiyo wilaya zilizo maskini, hivyo inawezekana kuna wilaya nyingine ambazo zinastahili kupata rasilimali zaidi. Chini ya AMV, mfumo ambapo sehemu ya mapato ya madini inatengwa kwa ajili ya jamii zinazoishi karibu na migodi unatarajiwa.

Kuna ushuru wa ndani (local levy) ambao makampuni ya uchimbaji madini yanatakiwa kulipa kwa kiasi cha 0.3% ya mapato na matumizi kwa mwaka na inalipwa kwa mamlaka ya Serikali ya Mitaa ambapo mgodi upo. Haya ni manufaa ya wazi kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa na hivyo kwa jamii zinazoishi karibu na mgodi. Hii inaendana na matarajio ya AMV. Kwa nyongeza, miradi ya Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR) nchini Tanzania inaweza pia kuhusishwa na sera, ingawaje imekuwa ikiendeshwa kama jambo la hiari kwa upande wa makampuni ya uchimbaji madini. Hata hivyo, kwa kutoa tamko kupitia sera, makampuni yanaweza kuendesha CSR kama njia yao ya kuonyesha kukubaliana kwao na sera ya Serikali. Nchini Tanzania, manufaa ya CSR pia yanaweza kuhusishwa na sera.

c. **Kuandaa utaratibu wa kuwezesha jamii kupata ajira, elimu, miundo mbinu ya usafiri, huduma ya afya, maji na usafi wa mazingira.**

Hakuna uamuzi wa kisera unaolazimisha makampuni ya uchimbaji madini kutoa kipaumbele kwa jamii katika utoaji wa ajira. Hata hivyo, jamii zimenufaika sana kwa kuwa na migodi katika maeneo yao kwa kupata ajira. Makampuni ya uchimbaji madini yamewekeza sana katika elimu, maji na mazingira, na afya. Wakati hili ni jambo chanya, haliwezi kuhusishwa na sera ya Serikali, kama inavyotarajiwa katika AMV. Ni muhimu kwamba Tanzania iwe na sera inayohimiza makampuni ya uchimbaji madini kutoa kipaumbele kwa jamii katika mipango mbalimbali, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ajira. Hili pia linatoka katika utafiti ulioandaliwa na Wizara ya Nishati na Madini, ambao ulionyesha kuwa wakati migodi imefanya juhudi inayostahili pongezi katika kuwajibika, matokeo ya juhudi zao zimekuwa kidogo, kwa sababu wangeweza kufanya zaidi, na mfumo wa utawala wa nchi pia unapaswa kulaumiwa, kwa kuzembea (Oxford Policy Management, 2011).

# 8. TATHMINI: KUOANISHA NA KUPANGA KWA KINA AMV KATIKA NGAZI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Mpango wa Utekelezaji wa AMV umeainisha viashiria vya ufuatiliaji ya ukanda wa Afrika Mashariki. Jumuiya ya Afrika Mashariki inategemewa:

i. Kufanya mapitio ya mazingira ya sasa ya fedha katika nchi za Afrika zinazoshughulika na uchimbaji ili kuandaa miongozo na viwango vya kuongeza mapato kadiri iwezekanavyo bila kudidimiza uwekezaji katika uchimbaji madini;
ii. Kuandaa miongozo ya kodi ya madini kwa ajili ya utekelezaji katika ngazi ya Jamii za Uchumi za Kikanda (RECs) na ngazi ya taifa;
iii. Kuandaa modeli za mifumo ya fedha kwa ajili ya miradi ya uchimbaji madini ya nchi wanachama na endesha warsha za mafunzo katika ngazi ya RECs na
iv. Kukusanya miongozo ya utendaji bora katika usimamizi wa mapato ya madini na zitawanye kwa utekelezaji katika ngazi ya REC na ngazi ya taifa.

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) imeshindwa kuandaa Hati ya Awali (Protocol) ya udhibiti wa sekta ya uchimbaji madini katika ngazi ya kanda, kutokana na Serikali ya Tanzania kukataa kutia sahihi Hati ya Awali. Kwa hiyo, Hati ya Awali haiwezi kutumika kama chombo cha kuoanisha na kupanga kwa kina AMV kwa kuwa haijapitishwa, ingawaje kuna baadhi ya mipango ambayo iko katika hati ya awali na inaenda sambamba na matarajio ya AMV. Lakini, ingawa hati hii ya awali bado haijapitishwa na nchi wanachama wote, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, pia imekuwa ikitekeleza baadhi ya shughuli ambazo zinafungamana na matarajio ya AMV. Kwa hiyo shughuli kama hizo zinaweza kuchukuliwa kama kitu chanya, kwani utekelezaji wake utasaidia katika kufanikisha baadhi ya matokeo tarajiwa ya AMV.

Mpango wa kuwezesha maendeleo ya viwanda vya uziduaji na uchakataji madini uko katika maandalizi hivi sasa. Mojawapo ya maeneo ya msisitizo ni mapitio ya sera na sheria zinazotawala viwanda vya uziduaji na uchakataji wa madini kusaidia maendeleo ya tasnia ya uziduaji madini na kuongeza thamani ya madini. Huu utaongeza ukusanyaji mapato kama ukifanikiwa, kwa hiyo unaendana na matarajio ya AMV. Kwa nyongeza, juhudi za kuoanisha sera ya madini na utawala katika nchi wanachama zinazotoa msisitizo katika ulipaji wa mirabaha kwa Serikali na jamii; utawala wa kodi; manufaa kwa jamii wakati na baada ya uchimbaji; wajibu wa jamii; mamlaka ya Serikali za Mitaa; Serikali Kuu na kampuni za uchimbaji madini; na uuzaji wa madini zinaendana na malengo ya AMV ya kuongeza mapato yanayotokana na sekta ya madini.

Hapajakuwa na majadiliano na mashauriano katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo yanalenga katika kujenga mifano / modeli ya usimamizi wa fedha kwa ajili ya miradi ya madini kwa nchi wanachama pia hakuna mafunzo yaliyotolewa kuhusu masuala hayo. Hapa ndipo mahali ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki iko mbali sana na matarajio ya AMV.

Pia ni muhimu sana kutambua kuwa viashiria vyote vya ufuatiliaji katika ngazi ya kanda viko katika mpango wa muda mfupi chini ya Mpango wa Utekelezaji wa AMV. Wakati kuna shughuli ambazo zimejadiliwa katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, utekelezaji wake kwa kiwango kinachotakiwa na AMV hautarajiwi kukamilika kwa mwaka 2016 (mwisho wa kipindi cha muda mfupi chini ya Mpango wa Utekelezaji wa AMV). Kwa kuwa hii mipango inayojadiliwa hapa bado haijawasilishwa kwa majadiliano na nchi wanachama. Kwa hiyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa haina mikakati inayoweza kutambulika kuwa inafungamana na matarajio ya AMV.

# 9. HITIMISHO

Utafiti wa kuoanisha na kupanga kwa kina utawala wa fedha za uchimbaji madini pamoja na usimamizi wa mapato yanayotokana na sekta hiyo kwa kutumia AMV kwa jumla umeonyesha kuwa kuna maeneo ambayo Tanzania imefanya vizuri sana, ingawa bado kuna masuala yanahitaji kutazamwa kwa karibu zaidi ukilinganisha na maeneo mengine. Maeneo ambako Tanzania imefanya vizuri kuhusu udhibiti wa fedha za uchimbaji madini ni pamoja na:

i. Tanzania baada ya miaka kadhaa, imeimarisha uwezo wake kitaifa wa kukagua kivitendo uzalishaji wa madini na mauzo nje ya nchi kwa kuunda shirika lenye uweledi la ukaguzi wa madini, TMAA. Matokeo yake ni utambuzi wa kodi ambazo zilikuwa bado hazijalipwa, wakati huo huo ikisaidia kujenga uwezo wa makampuni ya uchimbaji madini kukokotoa mapato ya kodi;
ii. Tanzania iliamua kufanya mabadiliko mengi katika mfumo wa kodi kwani tangu Sera ya Madini ya mwaka 2009, ambayo imeona mchango wa mapato ya kodi ya uchimbaji madini dhidi ya jumla ya mapato ya kodi yote yakiongezeka toka 2.41% mwaka 2001 hadi 4.41% mwaka 2014, hata katika kipindi ambapo bei za bidhaa katika soko la kimataifa zilikuwa zinashuka;
iii. Kumekuwa na mipango mingi ya kujenga uwezo inayolenga katika kuongeza uwezo wa maofisa wa Serikali kujadili mikataba ya uchimbaji madini na kufuatilia uhakika wa ufuataji wa sheria za kodi (udhibiti). Baadhi ya hii mipango ilisukumwa na AMDC, taasisi iliyoundwa ili kuongoza mpango wa AMV na
iv. Mamlaka ya Mapato Tanzania pia ilijaribu kuwa na utawala wenye ufanisi katika kuzuia uhawilishaji wa bei kwa kuandaa mwongozo wa uhawilishaji wa bei kuzuia uvujaji kwa kupitia uvujaji wa fedha ulio haramu. TMAA pia inatimiza kwa ufanisi wajibu wa kuzuia magendo ya madini na ukwepaji wa kodi ya madini.

Eneo moja hata hivyo, Tanzania bado inahitaji kuchukua hatua zaidi kuhusu mapitio ya masharti ya tozo la kodi maradufu na BITs ambayo Tanzania imetia sahihi na nchi wenyeji wa makampuni ya uchimbaji madini. Ingawa nchi imeweka sahihi idadi fulani ya BITs na DTTs, mfumo wa utawala umekuwa ukiwalinda sana wawekezaji. Kwa hiyo ni muhimu kwamba baada ya muda, mapitio yafanyike kuhakikisha kuwa mikataba bado inatimiza malengo. Mapitio kama haya ndiyo kitu kinachotakiwa na AMV.

Kuhusu matumizi ya mapato ya sekta ya uchimbaji madini na usimamizi wake, yafuatayo yanaweza kutamkwa kuhusu Tanzania:

a) Tanzania hivi sasa iko katika hatua za mbele katika kuanzisha mfuko maalumu wa matumizi ya mapato katika sekta ya madini katika muundo wa Mfuko wa Mapato ya Gesi Asilia, jambo ambalo linaendana na matakwa ya AMV. Hata hivyo, kuna hitaji la mifuko huru ya kiuchumi kuanzishwa pia kwa ajili ya madini mengine, kwa kuwa hizi ni rasilimali ambazo hatimaye zitaisha kuna umuhimu pia wa kuzingatia mahitaji ya vizazi vijavyo;

b) Utawala na usimamizi wa uchimbaji madini una utaratibu wa kuhakikisha kuwa makampuni ya uchimbaji madini yanalipa ushuru wa 0.3% ya mapato na matumizi kwa mwaka, ambayo hulipwa kwa mamlaka ya Serikali ya Mtaa ambapo mgodi upo. Hii inaonyesha kuwa udhibiti wa uchimbaji madini umejitahidi kuhakikisha kuwa kuna manufaa kwa mamlaka ya Serikali ya Mitaa na jamii zinazoishi karibu na mgodi, kama Mpango wa Utekelezaji wa AMV unavyotaka;

c) Tanzania haina mkakati wa kisera unaohimiza makampuni ya uchimbaji madini kutoa kipaumbele kwa jamii wakati wanapofanya uamuzi kuhusu ajira. Zaidi ya hayo, hakuna kanuni au utaratibu mahususi unaozitaka makampuni ya uchimbaji madini kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na madini kwa kuwekeza tena katika jamii ili kuimarisha afya, elimu na miundo mbinu kwa ujumla. Hivi sasa haya yanafanyika kwa hiari.

Katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, zoezi la kuoanisha na kupanga kwa kina (mapping) limeonyesha kuwa katika ngazi ya kanda mkakati uliopangwa umezuiwa kutokana na ukosefu wa maafikiano kati ya nchi wanachama kuhusu mkakati wa sekta ya uchimbaji madini. Matokeo yake, juhudi zinazofanyika katika ngazi ya mkoa hazifungamani moja kwa moja na matarajio ya AMV hasa katika eneo la utawala wa fedha za uchimbaji madini na usimamizi wa mapato, ingawa kuna jitihada zinafanyika katika ngazi ya sekretarieti ambazo zinastahili pongezi.

# 10. MAPENDEKEZO

Kutokana na matokeo ya uchunguzi, mapendekezo kadhaa yanaweza kutolewa kuharakisha hatua za kutekeleza matarajio ya AMV katika ngazi ya taifa na katika ngazi ya kanda. Katika ngazi ya taifa mapendekezo yafuatayo yanaweza kufanyika:

i. Tanzania inahitaji kuendeleza hizi juhudi za sasa za kuandaa dira ya taifa ya uchimbaji madini inayofungamana na AMV. Ari iliyotokana na juhudi za sasa katika ngazi ya Serikali kwa kushirikiana na AMDC isipotee bure. Asasi za kiraia kama vile Mtandao wa Haki Kodi (Tax Justice-Network) zinaweza kuunda maeneo ya mipango yao kuendana na AMV ili kuhakikisha kuwa juhudi hizi zinaendelezwa;

ii. Tanzania inahitaji kuendelea kuhakikisha kuwa uwezo wa ukaguzi wa madini ambao umejengeka ndani ya TMAA, unaimarishwa muda wote kusudi uwezo huo wa ukaguzi uendane na mikakati inayoendelea kuibuka kuhusu mitiririko haramu ya fedha inayotumiwa na watu katika sekta ya madini. Kuna hitaji la kuhamasisha wadau wote kuhusu umuhimu wa kuendelea kuimarisha uwezo huo;

iii. Tanzania inapaswa iendelee kutumia msaada wa AMDC katika maeneo mengine ya mapato ya sekta ya uchimbaji, ikijumuisha uwezo wa kujadili vibali vya kuchimba madini pamoja na utawala bora kuhusu BITs na mikataba ya tozo la kodi maradufu kuhakikisha kuwa nchi inapata au inafikia kiwango cha juu cha udhibiti bora wa uchimbaji madini kama inavyotarajiwa chini ya AMV;

iv. Tanzania pia iendelee kuonyesha msimamo na ari ile ile iliyokuwa nayo katika uanzishaji wa mfuko maalumu wa matumizi ya mapato kwa ajili ya sekta ya gesi, katika uanzishaji wa mifuko kama hiyo kwa madini mengine. Madini mengine nayo pia yana umuhimu sana, na mantiki iliyotumika kwa sekta ya gesi inaweza ikatumika pia kwa madini mengine yote na

v. Pamoja na ushuru wa ndani, Tanzania pia inahitaji kuandaa mkakati wa kisera kuhakikisha kuwa jamii zinazoathirika kutokana na shughuli za uchimbaji madini hususan uchafuzi wa hali ya hewa na mazingira, nazo zijisikie kuwa sehemu ya miradi ya uchimbaji madini. Sehemu ya mapato yanayotokana na uchimbaji madini inaweza kuwekezwa tena katika jamii kupitia miradi yenye lengo la kuboresha afya, elimu, maji na usafi wa mazingira

Katika ngazi ya kanda, inapendekezwa kuwa kuna hitaji la haraka la kuandaa mkakati wa uchimbaji madini unaokubalika na nchi wanachama wote. Kwa nyongeza, sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ichukue fursa inayotokana na Tanzania kukataa kuweka sahihi hati ya awali (protocol) ya sasa kwa kutengeneza mkakati mpya unaooanisha na kupanga kwa kina AMV na vipengele vyake vyote, ikijumuisha mapato ya fedha zinazotokana na uchimbaji madini na udhibiti wake. Uwepo wa AMV unasaidia kwa kuibua masuala ambayo ni ya manufaa kwa nchi zote, na ambayo nchi wanachama wote wamekubaliana.

# MAREJEO

Bank of Tanzania (BOT), Tanzania Investment Centre (TIC) and National Bureau of Statistics (NBS). (2013). 'Tanzania Investment Report, Foreign Private Investment', found online at website http://www.tic.co.tz/menu/196?l=en.

Baunsgaard, T. (2014). 'Tanzania: Recent Economic Developments and Outlook.' Presentation made at REPOA by Thomas Baunsgaard, Resident Representative, International Monetary Fund, April 2014.

Jumuiya ya Afrika Mashariki. (2013). '5th Meeting of the 1st Session of the East African Legislative Assembly, Kigali, Rwanda, 12th – 26th April 2013', East African Community, 18th April 2013.

ESRF. (2014). Tanzania Sovereign Wealth Fund. The Economic and Social research Foundation TAKNET Policy Brief Series No. 020 – 2014.

ICMM. (2009). The Challenge of Mineral Wealth: Using resource endowments to foster sustainable development. London: International Council on Mining and Metals in association with the Commonwealth Secretariat.

IMF. (2014). United Republic of Tanzania: Selected Issues. Washington, D.C: International Monetary Fund.

MoEM. (2015). Tanzania Mining Industry Investor's Guide. Dar es Salaam: Ministry of Energy and Minerals.

Oxford Policy Management. (2011), 'Investments Benefits Study', Paper prepared for the Ministry of Energy and Minerals under the Sustainable Management of Mineral Resources project (SMMRP).

Poncian, J. (2015), 'Mineral Extraction for Socio-Economic Transformation of Tanzania: The Need to Move from Papers to Implementation of Mining Policy and Law', Journal of Social Science Studies. 2015, Vol. 2, No. 2.

PricewaterhouseCoopers. (2012). 'Corporate income taxes, mining royalties and other mining taxes: A summary of rates and rules in selected countries', a PwC 2012 update.

TEITI. (2014). 'Press Release on Launching of the 4th Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative: Reconciliation of payments made by Extractive companies and Revenues received by government from Extractive companies', Tanzania Extractive Industries Initiative, 2015.

TEITI. (2015). Sixth Report of the Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative for The Year Ended 30 June 2014. Dar es Salaam: Tanzania Extractive Industries Initiative.

TMAA. (2015). TMAA Annual Report, 2014. Dar es Salaam: Tanzania Minerals Audit Agency.

UNCTAD. (2014) Treaty Database – Bilateral Investment Treaties signed by Tanzania, available at http://unctad.org/Sections/dite_pcbb/docs/bits_tanzania.pdf. Accessed on 28/01/2016.

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho 1: Maelezo ya jinsi uoanishaji na upangaji wa kina (mapping) wa AMV kwa Tanzania ulivyofanyika**

| Matokeo Tarajiwa | Shughuli | Muda | Hali kwa Tanzania |
|---|---|---|---|
| Ongezeko la gawio ya mapato ya madini kwa nchi za Kiafrika zinazoshughulika na uchimbaji madini. | Boresha uwezo wa taifa wa kukagua kwa vitendo uzalishaji na uuzaji madini nje ya nchi | ST | Uwezo wa taifa wa kukagua kivitendo uzalishaji wa madini na mauzo nje ya nchi uliongezwa na shirika lenye uweledi la ukaguzi wa madini, TMAA. Hii, matokeo yake ni utambuzi wa kodi ambazo zilikuwa bado hazijalipwa, wakati huo huo ikisaidia kujenga uwezo wa makampuni ya uchimbaji madini kukokotoa mapato ya kodi. |
| | Fanya mapitio ya utawala wa madini kwa lengo la kuongeza mapato | ST | Tanzania imefanya mabadiliko mengi katika mfumo wa kodi kwani tangu sera ya Madini ya mwaka 2009, ambayo imeona mchango wa mapato ya kodi ya uchimbaji madini dhidi ya jumla ya mapato ya kodi yote yakiongezeka toka 2.41% mwaka 2001 hadi 4.41% mwaka 2014, hata katika kipindi ambapo bei za bidhaa katika soko la kimataifa zilikuwa zinashuka. |
| | Jenga uwezo na ongeza stadi za maofisa katika kujadili masuala ya fedha na kufuatilia kwa ufanisi ufuataji wa sheria za kodi. | ST-MT-LT | Kumekuwa na mipango mingi ya kujenga uwezo inayolenga katika kuongeza uwezo wa maofisa wa Serikali kujadili mikataba ya uchimbaji madini na kufuatilia uhakika wa ufuataji wa sheria za kodi (udhibiti). Baadhi ya hii mipango ilisukumwa na AMDC, taasisi iliyoundwa ili kuongoza mpango wa AMV. |
| | Jadili au jadili tena mikataba kuongeza mapato hadi upeo wa juu kabisa na kuhakisha nafasi ya fedha usimamizi wa mapato yasiyotegemewa | ST-MT | Tanzania imefanya leseni nyingi ziweze kupatikana kwa upya (ya zamani inapoisha muda wake), na wakati wa kuomba leseni mpya masharti mapya yanajadiliwa siku zote kutegemea sera ya madini inayotumika wakati huo. Lakini, MDAs zinaweza kufanya baadhi ya makampuni zisiweze kufanyiwa majadiliano kwa upya kwa kipindi cha miaka 10. |
| | Unda mifumo ya kutathmini vipengele vya utawala wa kodi kwa kuchunguza uvujaji, upotevu na ukwepaji na uepukaji kodi (k.m. uhawilishaji bei). | ST-MT | Mamlaka ya Mapato Tanzania pia ina mwongozo wa uhawilishaji wa bei, wakati Kanuni za Kodi ya Mapato (Uhawilishaji bei) za mwaka 2014 zilitungwa ili kuzuia uvujaji wa fedha ulio haramu kupitia uhawilishaji bei. TMAA pia inatimiza kwa ufanisi wajibu wa kuzuia magendo ya madini na ukwepaji wa kodi ya madini. |
| | Kurejea masharti ya mikataba ya utozaji kodi mara mbili (BITs) pamoja na nchi wenyeji wa makampuni ya uchimbaji madini ikijumuisha kanuni ya madini kutozwa kodi katika hatua ya uziduaji. | ST-MT | Tanzania imetia sahihi BITs na nchi 14, ingawa majadiliano na nchi nyingine zaidi yanaendelea hivi sasa. Tanzania pia imetia sahihi mikataba ya tozo la kodi maradufu na nchi 14. Mfumo wa utozaji kodi Tanzania bado umeundwa ili kuhakikisha kuwa kodi inalipwa Tanzania, hata kama wawekezaji wa nje wanahusika. Lakini masharti ya mikataba iliyowekewa sahihi haijafanyiwa mapitio mara kwa mara. |
| | Jenga uwezo na mifumo ya kunadi haki za madini pale inapowezekana. | ST | Wakati mfumo wa utoaji leseni uko wazi, vipengele vinavyotumika kabla ya utoaji wa kibali kwa mwekezaji, hususan kama kuna wawekezaji zaidi ya wawili wenye kuhitaji kibali havijawekwa wazi. Ni vigumu kuondoa uwezekano wa ushawishi au athari nyingine kuingilia kati maamuzi ya utoaji vibali (concessions). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kuboreshwa kwa usimamizi na matumizi ya mapato yanayotokana na madini | Chunguza mikakati ya kuwekeza mapato yasiyotegemewa, mapato ya kawaida na renti ya madini katika mfuko huru wa kiuchumi ikiwa ni pamoja na mfuko wa udhibiti na mfuko wa miundo mbinu. | ST | Tanzania hivi sasa iko katika hatua za mbele katika kuanzisha mfuko maalumu wa matumizi ya mapato katika sekta ya madini katika muundo wa Mfuko wa Mapato ya Gesi Asilia, jambo ambalo linaendana na vijfungu vya AMV. Hata hivyo, kuna hitaji la mifuko huru ya kiuchumi kuanzishwa pia kwa ajili ya madini mengine, kwa kuwa hizi ni rasilimali ambazo hatimaye zitaisha kuna umuhimu pia wa kuzingatia mahitaji ya vizazi vijavyo. |
| | Andaa mifumo ya kusambaza renti ili kugawa sehemu ya mapato yanayotokana na madini kwa jamii na mamlaka za jamii zinazoishi jirani na migodi | ST | Utawala na usimamizi wa uchimbaji madini una utaratibu wa kuhakikisha kuwa makampuni ya uchimbaji madini yanalipa ushuru wa 0.3% ya mapato na matumizi kwa mwaka, ambayo hulipwa kwa mamlaka ya Serikali ya mitaa ambapo mgodi upo. Hii inaonyesha kuwa utawala wa uchimbaji madini umejitahidi kuhakikisha kuwa kuna manufaa kwa mamlaka ya Serikali ya mitaa na jamii zinazoishi karibu na mgodi, kama Mpango wa Utekelezaji wa AMV unavyotaka |
| | Andaa mipango ya kuwezesha jamii husika kupata kazi, elimu, miundo mbinu ya usafiri, huduma ya afya, maji na usafi wa mazingira | ST-MT | Tanzania haina mkakati wa kisera unaohimiza makampuni ya uchimbaji madini kutoa kipaumbele kwa jamii wakati wanapofanya maamuzi kuhusu ajira. Zaidi ya hayo, hakuna kanuni au utaratibu mahususi unaozitaka haya makampuni ya uchimbaji madini kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na madini kwa kuwekeza tena katika jamii ili kuimarisha afya, elimu na miundo mbinu kwa ujumla. Hivi sasa haya yanafanyika kwa hiari. |
| | Jenga uwezo wa jamii kujadili mikataba ya ushirikiano | MT | Hivi sasa hakuna maamuzi yo yote ya kisera yanayotaka jamii iwe na hisa katika maeneo ya uchimbaji madini. Kwa hiyo mikataba ya ubia kati ya jamii na makampuni ya uchimbaji madini haitambuliki kisheria. |
| | Andaa mifumo ya kujenga uwezo wa vyombo / taasisi za taifa na za chini yake kusimamia mapato. | MT | Tanzania ina vyombo/taasisi imara kitaifa zenye ufanisi katika usimamizi wa mapato |

**Kiambatanisho 2: Tanzania kadi ya alama kuhusu ngazi ya utekelezaji wa AMV**

| Matokeo Tarajiwa | Shughuli | Alama kwa Tanzania (5 ni alama ya juu na sifuri ni alama ya chini). 5 inaonesha mfungamano kabisa na AMV wakati sifuri inaonesha kuwa hakuna mfungamano wo wote na AMV |
|---|---|---|
| Ongezeko katika mgawo wa mapato yanayotokana na madini kwa nchi za kiafrika zinazoshughulika na uchimbaji madini. | Boresha uwezo wa taifa wa kukagua kwa vitendo uzalishaji na uuzaji madini nje ya nchi | 4 |
| | Fanya mapitio ya utawala wa madini kwa lengo la kuongeza mapato kadiri iwezekanavyo | 4 |
| | Jenga uwezo na ongeza stadi za maofisa katika kujadili masuala ya fedha na kufuatilia kwa ufanisi ufuataji wa sheria za kodi. | 4 |
| | Jadili au jadili tena mikataba kuongeza mapato hadi upeo wa juu kabisa na kuhakisha nafasi ya fedha na usimamizi wa mapato yasiyotegemewa | 2.5 |
| | Unda mifumo ya kutathmini vipengele vya utawala wa kodi kwa kuchunguza uvujaji, upotevu na ukwepaji na uepukaji kodi (k.m. uhawilishaji bei). | 3 |
| | Kurejea masharti ya mikataba ya utozaji kodi mara mbili (BITs) pamoja na nchi wenyeji wa makampuni ya uchimbaji madini ikijumuisha kanuni ya madini kutozwa kodi katika hatua ya uziduaji. | 2 |
| | Jenga uwezo na mifumo ya kunadi haki za madini pale inapowezekana. | 2.5 |
| Uboreshaji wa usimamizi na matumizi ya mapato ya madini. | Chunguza mikakati ya kuwekeza mapato yasiyotegemewa na renti ya madini kwenye mifuko huru ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na Mifuko ya udhibiti na mifuko ya miundo mbinu. | 3 |
| | Andaa mifumo ya kusambaza renti ili kugawa sehemu ya mapato yanayotokana na madini kwa jamii na mamlaka za jamii zinazoishi jirani na migodi | 3 |
| | Andaa mipango ya kuwezesha jamii husika kupata kazi, elimu, miundo mbinu ya usafiri, huduma ya afya, maji na usafi wa mazingira | 2 |
| | Jenga uwezo wa jamii kujadili mikataba ya ushirikiano | 2 |
| | Andaa mifumo ya kujenga uwezo wa vyombo / taasisi za taifa na za chini yake kusimamia mapato. | 4 |